Nipashe
Jumatano Aprili 22, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580212
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
...lian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



## TOLEO MAALUM: Dk. Reginald Mengi ameonyesha uzalendo

UKURASA 3


Wanahabari walioandaliwa ni muhimu Uchaguzi Mkuu Ukurasa 13

siasa
JUMATANO APRILI 22, 2020
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

Corona yawatia lawamani viongozi Ulaya, Marekani Ukurasa 14

Na Beatrice Moses

AJUAYE ni Mungu jinsi Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Assemblies of God Mikocheni B. Mlima wa Moto, Dk. Gertrude Rwakatare, alivyoingia kwenye siasa na kufanikiwa kuwa mbunge wa viti maalum, akiwa amebeba ujumbe wa Injili kila alipisimama.

Bungeni Dodoma kwenye vikao, karibu mara zote alipochangia hoja hakuionea haya Injili japo maneno machache. Bunge litakosa mahubiri huyu shujaa.

KUPATA UBUNGE

Ilikuwa mwaka 2005 alijitokeza kugombea ubunge kwa tiketi ya viti maalum, hata hivyo kura hakufanikiwa wakati huo hadi mwaka 2007 baada ya kifo cha aliyekuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Salome Joseph Mbatia.

Mbatia alikuwa ni Mbunge Viti Maalumu CCM aliyefariki kwa ajali ya gari Njombe mkoani Iringa, akiwa kwenye kampeni za kusaka ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa.

Dk. Rwakatare licha ya kuwa Askofu mbunge, pia alikuwa ni mmiliki wa Shule za St Mary's International na katika shughuli za uwekezaji alisifika kwa kiwango kikubwa ikiwamo kuwekeza kwenye maisha ya wahitaji na pia kina mama wengi.

Aidha, anatajwa kuwa mpenda watu na Februari mwaka huu, mbunge huyu wa viti maalum jimbo la Kilombero, alikabidhi pikipiki 22 kwa CCM ili zitumike kwenye kampeni za uchaguzi.

Awali alieleza kuwa alishakabidhi baskeli 300 kwa chama hicho ili kukisaidia kuleta maendeleo jimboni Kilombero.

Historia ya maisha ya kisiasa inaonyesha kuwa mwaka 2010 alishinda ubunge wa viti maalumu japo 2015 hakupata nafasi hiyo hadi 2017 alipoteuliwa kuziba nafasi ya Mwenyekiti wa UWT Sophia Simba, baada ya kuvuliwa uanachama CCM.

MAOMBI MAALUMU

Katika michango yake bungeni

Dk. Rwakatare muda mfupi baada ya kukabidhi pikipiki kwa Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ali, (mwenye kofia ngumu) wilayani Kilombero mapema mwaka huu. PICHA: BLOGI YA CCM

Buriani Dk. Rwakatare; Mchungaji, mbunge

"Mheshimiwa Spika, naomba nyumba za askari Ifakara na Kilombero zijengwe, wana shida kubwa ya makazi."

ilidhihirisha nguvu ya kuhubiri ilivyokuwa ndani yake, wakati akichangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji, alianza: "Awali ya yote ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema yeye ambaye ametupa zawadi ya uhai, ametupa zawadi ya afya, ametupa zawadi ya maji, ametupa zawadi ya ulinzi, na hakika tunasafiri na kurudi kwa sababu ya ulinzi wake. Mungu wetu ni mwema."

"...Ningependa kuchukua nafasi hii kumweka kila mmoja wetu hapa mikononi mwa Mungu aweze kuwatetea na kuwalinda kwenye majimbo yenu, kazi zenu ziweze kwenda salama."

"Lakini zaidi tuombe maombi rasmi kwa ajili ya Rais wetu John Magufuli, hakika kabisa tumepata chuma, tumepata jembe, lakini tumepata baba yeye...." alisema na kuongeza kuwa anaomba Rais apate kibali kwa Watanzania wote na jina lake liwe sukari midomoni, chumvi midomoni mwao na ulinzi wa Mungu uwe juu yake kwa jina la Yesu.

DOKTA MENGI

Dokta Rwakatare, alimkumbuka mfanyabiashara maarufu, Dk. Mengi, akisema "Nachukua pia nafasi hii niweze kumkumbuka mheshimiwa Dk. Reginald Mengi, mfanyabiashara maarufu. Tukikumbuka katika bajeti ya maji, ndiye aliyeanzisha maji ya chupa Kilimanjaro, ameanzisha ITV, mambo mengi amefanya, ana huruma anakula na watu wenye shida, walemavu, kwa hivyo amefanya kazi nzuri Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi

Akichangia hotuba hiyo anasisitiza kuwapunguzia wanawake mzigo wa kusaka maji... "ningependa nijikite kwenye maji safi na salama mnajua maji ni kila kitu na lengo letu ni kumtua mwanamke ndoo ili aweze kupumzika maji yafike nyumbani.

Alibainisha kuwa anatokea Morogoro kwenye mito 177 ya kudumu na sio ile msimu, pia katika Wilaya ya Kilombero kuna mito 38 ya kudumu ya kudumu na ikujumlishwa ni mingi.

" Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba watu wengi hawajafikiwa na majisafi na salama inabidi wakachote mtoni, wakatafute ni shida. Lakini nilikuwa naomba katika bajeti hii Waziri utuhurumie watu wa Kilombero uweze kuangalia kwa maana maji yapo Mungu ametupa neema tatizo kubwa ni miundombinu

Tunaomba Waziri aiangalie Kilombero kwa huruma, tumevumilia miaka mingi. Nakumbuka ya kwamba miundombinu ile ilikuwa kama Ifakara mjini ilihudumia watu 7,000 enzi hizo sasa hivi watu ni takribani 300,000 mji wa Ifakara pekee. Kwa hivi tunaomba kwa kweli mtusaidie na sisi tupate majisafi na salama."

POLISI IFAKARA

Wakati akichangia mapato na makadirio ya fedha kwa mwaka 2019/2020 kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi -Rwakatare, licha ya kupongeza utendaji kazi wa polisi anaomba wajengewe nyumba.

"Mheshimiwa Spika, naomba nyumba za askari Ifakara na Kilombero zijengwe, wana shida kubwa ya makazi."

Pia aliomba Mahakama ya Ifakara ijengwe kwa kuwa, wakati wa masika mafuriko yanaathiri wafungwa, mafaili, ofisi, hivyo ni kero kubwa.

Dk Rwakatare alipenda elimu na alikaririwa akichangia pia kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Dk. Bashiru: Kugawa sukari na vitenge ni matusi kwa mpigakura Ukurasa 12

UKURASA 11

### TISHIO LA CORONA

# Mwili wa Rwakatare kutopelekwa bungeni

• **Spika** asema utazikwa kesho eneo la kanisa na watu wasiozidi 10... *Endelea ukurasa wa 2*



### BAA LA CORONA

**Ukijisikia mwili kuuma unashauriwa kukaa nyumbani kama hakuna ulazima wa kutoka. Kama una homa, unakohoa na kupata shida wakati wa kupumua, tafuta msaada wa kitabibu. WHO**
- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akipita katika mashine maalum ya kunyunyizia yenye dawa ya kujikinga na virusi vya corona alipoingia kwenye viwanja vya Bunge jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

## Wastaafu kuandaliwa mafao miezi sita kabla

UKURASA 2

## TLS yataka mambo 26 Corona

UKURASA 2

Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
GET IT ON Google Play
Download on the App Store

MICHEZO VITA YA VIUNGO YAKOLEA YANGA UK.24
MAONI, KATUNI UK.6

# Corona yakwamisha mwili wa Rwakatare kupelekwa bungeni

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

UONGOZI wa Bunge umesema aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Askofu Getrude Rwakatare (70), hataagwa kwenye viwanja vya Bunge kama ilivyo kawaida kutokana na mlipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha homa ya mapafu.

Umesema unawasiliana na familia ili kujua utaratibu wa mazishi na ndipo Bunge litajulishwa namna wabunge watakavyoshiriki kumuaga mwenzao.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliyasema hayo jana, alipotoa taarifa hiyo bungeni jijini hapa na kuwataka wabunge kuwa na subira wakati huu.

"Tunaendelea na mawasiliano na familia, kwa kawaida mbunge akifariki (dunia), wakati vikao vya Bunge vikiendelea, tunaacha kikao kimoja, tunamleta hapa (bungeni) tunamuaga kwa pamoja, lakini kwa mazingira ya sasa ya corona, hatutaweza kumleta hapa,"alisema.

"Maelezo mengine yatapatikana kesho (leo) baada ya kumaliza mazungumzo kati ya familia na Bunge," Spika Ndugai alisema.

Hata hivyo, jana jioni, Spika Ndugai alitangaza bungeni kuwa mwili wa mbunge huyo utazikwa kesho kwenye eneo le kanisa jijini Dar es Salaam.

Kiongozi huyo wa Bunge alisema serikali itasimamia mazishi hayo na washiriki hawatazidi 10.

Spika Ndugai aliwataka wabunge kukubaliana na uamuzi wa serikali na familia katika suala hilo.

Dk. Rwakatare ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Morogoro, alifariki Aprili 20 mwaka huu, akipata matibabu katika Hospitali ya Rabinisia, Tegeta jijini Dar es Salaam. Alikuwa Askofu wa Kanisa la Mikocheni B Assemblies of God, maarufu Mlima wa Moto.



Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi na Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Shaaban Seif Mohammed wanaonekana kwenye skrini wakizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa Vodacom Tanzania PLC, Hisham Hendi na Mkurugenzi wa Vodacom Tanzania Foundation, Rosalynn Mworia, kampuni hiyo ilipokabidhi shilingi milioni 300 kwa serikali ya Mapinduzi Zanzibar jana, ili kupambana na kudhibiti ongezeko la virusi vya corona visiwani humo. Makabidhiano hayo yalifanyika kwa njia ya mtandao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TLS yataka mambo 26 corona

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Wanasheria Tanganyika (TLS), kimetoa mapendekezo 26 kwa serikali kupambana na maambukizi ya virusi vya corona ikiwamo kuwekwa karantini watu wote na kuwazuia kutoka kwenye nyumba zao kwa siku 21.

Kwa mujibu wa taarifa ya Rais wa chama hicho, Dk. Rugemeleza Nshala, wanapendekeza serikali ichukue hatua hizo ili kuzuia kuendelea kusambaa kwa ugonjwa huo.

Pia, kimependekeza kuwapo mkakati maalum wa kupima wananchi ili kubaini wenye maambukizi kama zilivyofanya nchi za Rwanda, Kenya, Uganda, Korea Kusini na Ujerumani.

Chama hicho pia kimependekeza mahakama ziahirishe kusikiliza kesi kwa kipindi cha siku 30 na kuendelea na zile ambazo zinaweza kusikilizwa kwa njia ya mtandao.

"Tunapendekeza kunyunyizia dawa katika miji na mitaa mbalimbali hapa nchini ili kuua virusi wa ugonjwa wa corona. Kuanzishwa mpango maalumu wa kugawa na kusambaza vyakula kwa familia zenye uwezo mdogo wakati wote wa kipindi cha karantini ya siku 21," chama hicho kilishauri.

Pia, TLS kimependekeza serikali itoe msamaha wa kulipa mikopo na marejesho ya malipo ya mikopo kwa muda wa miezi mitatu kwa watu waliokopa kutoka taasisi za fedha nchini.

"Serikali ihakikishe vifaa vya kujikinga na ugonjwa huu vinagawiwa na kusambazwa kwa wananchi bure au kwa bei nafuu kabisa. Serikali iandae na kutekeleza mkakati maalum wa kuziokoa sekta za kiuchumi nchini ambazo zimeathiriwa kutokana na baa la ugonjwa huu.

"Kuzuia kutozwa kodi ya pango kwa waajiri na wafanyabiashara kwa kipindi cha miezi mitatu kama njia ya kutoa nafuu kwa waajiri na wafanyabiashara kutokana na mdororo wa uchumi uliosababishwa na baa la ugonjwa wa korona," kimependekeza.

Pia chama hicho kinataka kuboreshwa mfumo wa afya jamii ili kuwezesha kukabiliana na milipuko ya pili na ya tatu ya ugonjwa huo.

"Serikali iombe msaada kutoka taasisi za kidunia na nchi kupata rasilimali fedha za kupambana na corona pamoja na kusamehewa kulipa madeni yake kutokana na uchumi wake kuathiriwa kwa baa hili," kimependekeza chama hicho.

TLS kimependekeza waajiri kuweka utaratibu wa wafanyakazi wa kufanya kazi wakiwa nyumbani kwa shughuli zile ambazo zinaweza kufanywa wakiwa huko ili kupunguza kuparaganyika kwa uchumi.

"Kuondolewa magerezani mahabusi ambao makosa yao yanadhaminika na wale ambao walizuiwa kupewa dhamana kutokana na Mkurugenzi wa Mashitaka kuweka hati ya kuzuiwa dhamana zao," kimesema.

Chama hicho pia kimependekeza kutolewe msamaha wa Rais kwa wafungwa ambao wanakaribia kumaliza muda wao na wale ambao makosa yao siyo ya mauaji, ubakaji, wizi wa kutumia nguvu na dawa za kulevya kama heroin.

# Mafao kuandaliwa miezi 6 kabla kustaafu

**Na James Mwanamyoto,** DODOMA

OFISI ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imepanga kukutana na maofisa Utumishi wote nchini kuwakumbusha na kuwasisitiza umuhimu wa kuandaa mapema taarifa za mtumishi anayetarajia kustaafu miezi sita kabla ya kustaafu kuondoa tatizo la ucheleweshwaji wa mafao ambao baadhi yao hufariki bila kuyapata.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, alisema hayo alipokuwa akitoa ufafanuzi wa namna atakavyotekeleza ahadi aliyoitoa bungeni ya kuhakikisha ofisi yake inatatua changamoto ya ucheleweshwaji wa mafao ya wastaafu wakati akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mkuchika alisema, anakwazwa na kitendo cha wastaafu walioitumikia nchi kwa uadilifu kuchelewa kupata mafao yao kwa wakati.

"Nasononeshwa na kitendo cha wastaafu walioitumikia nchi kwa uadilifu na uzalendo kucheleweshewa mafao yao kwa muda mrefu, kuanzia mwaka mmoja hadi minne na wengine kufariki bila kupata mafao yao," Mkuchika.


Alisema katika kipindi cha uongozi wake amebaini kuwa tatizo la wastaafu kuchelewa kupata mafao linasababishwa na baadhi ya maofisa utumishi kuchelewa kuandaa taarifa za wastaafu mapema na kuziwasilisha kwenye mamlaka husika, ikiwa ni pamoja na kitendo cha baadhi ya waajiri kutowasilisha michango ya watumishi kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii.

Vile vile, amewapiga marufuku maofisa hao kuwaelekeza wastaafu kufuatilia mafao yao jijini Dodoma au Dar es Salaam na badala yake wao ndio wabebe jukumu hilo kwa kuwa wastaafu wengi wanapata usumbufu na kukabiliwa changamoto ya ukosefu wa fedha.

Alitoa rai kwa maofisa hao kuwajibika ipasavyo na ikitokea mstaafu amechelewa kupata mafao yake, Ofisa Utumishi ndiye atatakiwa kuieleza serikali sababu za mstaafu huyo kutopata mafao yake kwa wakati, ikizingatiwa kuwa serikali imeshawaelekeza maofisa hao kuandaa taarifa za watumishi wanaotarajiwa kustaafu mapema iwezekanavyo.

Alisema ofisi yake inahusika na utawala bora hivyo itahakikisha mstaafu analipwa stahili zake kwa wakati na kitendo cha mstaafu kukaa miaka minne bila kulipwa mafao hakiakisi dhana halisi ya utawala bora.

Tatizo la kutopata mafao kwa wakati limekuwa likiwaathiri wastaafu ambao wanashindwa kufurahia matunda ya utumishi wao na serikali imedhamiria kutatua changamoto ya ucheleweshwaji kwa kukutana na maofisa utumishi ili kuweka mkakati wa kuondokana na tatizo hilo.



TOLEO MAALUM

## DK. REGINALD ABRAHAM MENGI

"Unaweza kubadilisha maisha yako endapo utakuwa na imani ya dhati ya vile unavyotaka kuwa."

# Ameonyesha uzalendo

**Na Gwamaka Alipipi**

MWENYEKITI Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, alijitoa kuwasaidia watu wenye ulemavu nchini na kupitia kampuni zake alihakikisha watu hao wanapata ajira na hata ilipotokea tatizo la kuyumba kwa uchumi na kuhitajika baadhi ya wafanyakazi kupunguzwa kazini, jamii ya watu hao haikuguswa.

**CHAKULA NA WENYE ULEMAVU**

Kila mwaka Dk. Mengi aliandaa chakula cha mchana kilichokuwa kikiwakutanisha watu wote wenye ulemavu na alishiriki kula nao kwa kualika pia viongozi wa juu wa kitaifa kusherehekea siku hiyo.

Katika chakula hicho cha mchana pia aliandaa burudani mbalimbali zikiwamo muziki ili watu wa jamii hiyo nao wasijione wametengwa na kuwa sawa na binadamu wengine wenye viungo kamili.

Hakujali cheo chake, alijishusha kwa kuonyesha upendo na utu kwa watu hao kwa kuungana na wafanyakazi wengine wa IPP kuwahudumia walioshindwa kwenda kuchukua chakula kwa kuwabebea sahani za chakula na kuwapelekea kwenye meza zao.

Aliwasadia wasionacho na wenye uhitaji kwenye jamii ikiwamo watu wenye ualbino.

**MSAADA WA VIFAA**

Alifadhili upatikanaji wa vifaa tiba na vinavyorahisisha kukabili yanayowasibu watu wenye ulemavu.

Kwa mfano, upatikanaji wa miguu bandia, baiskeli za miguu mitatu, pamoja na fimbo nyeupe. Yote aliyafanya kuonyesha upendo na kuwajali watu wa kundi hilo.

Aliwaona ni sehemu ya watoto wake, wakati wote aliwasikiliza na kuwajali, aliwasaidia, hakupenda kuwaona wakipata tabu.

Aliwasaidia mtu mmoja mmoja, vyama vya kutetea sera na mustakabali wa watu wenye ulemavu.

Alikuwa akitoa elimu kwa umma wa Watanzania na kupinga vitendo vya ukatili kwa watu wenye ulemavu kupitia vituo vyake vya habari, yaani televisheni, redio, magazeti ambavyo vilikuwa mstari wa mbele kukemea vitendo vya ukatili kwa watu hao.

Pia, Dk. Mengi alikuwa akifadhili kwa muda mrefu shughuli za kiuchumi kwa watu wenye ulemavu na kufadhili safari na kuhudhuria mikutano ya ndani nan je ya nchi kwa viongozi wawakilishi wa watu wenye ulemavu.



Dk. Reginald Mengi akiwahudumia chakula watu wenye ulemavu waliohudhuria katika hafla ya chakula cha mchana katika ukumbi wa Diamond Jubilee, jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

> Aliwaona ni sehemu ya watoto wake, wakati wote aliwasikiliza na kuwajali, aliwasaidia, hakupenda kuwaona wakipata tabu.



**TANGAZO**

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

UBA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 31.03.2020

**Imetolewa chini ya kanuni ya 32 kifungu namba 3 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2006**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31-Machi 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya 31-Mar-20 | Robo Mwaka ya 31-Dec-19 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 3,702 | 2,008 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 11,210 | 9,947 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 89,053 | 86,828 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 2,407 | 4,976 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 72 | 1,970 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 60,591 | 68,236 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 43,903 | 42,181 |
| 12 | Mali Nyingine | 5,465 | 8,951 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,448 | 1,538 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **217,852** | **226,635** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 69,021 | - |
| 18 | Amana za Wateja | 110,028 | 111,095 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 7,696 | 8,157 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,105 | 674 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 7,600 | 8,708 |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,439 | 5,020 |
| 28 | Madeni | - | 3,510 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **196,889** | **137,164** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **20,963** | **89,470** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,420 | 31,420 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 29,104 | 29,104 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (40,582) | (42,166) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,021 | 1,668 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **20,963** | **20,026** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 848,291 | 841,483 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 3,933 | 234 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 709 | 891 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 10% | 9% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 8.90% | 0.55% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 38% | 33% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 20% | 19% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 89% | 88% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -1% | -7% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -4% | -6% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
### KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31-Machi 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 31-Mar-20 | Robo ya Mwaka linganishi 31-Dec-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mar-20 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Mar-19 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 3,958 | 4,423 | 3,958 | 1,897 |
| 2 | Gharama za Riba | (1,510) | (1,702) | (1,510) | (682) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **2,447** | **2,722** | **2,447** | **1,214** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | (298) | - | - |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **2,323** | **1,584** | **2,323** | **2,178** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 307 | 371 | 307 | 409 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 1,998 | 1,199 | 1,998 | 1,736 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 18 | 14 | 18 | 33 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(3,749)** | **(3,421)** | **(3,749)** | **(3,352)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (1,794) | (1,658) | (1,794) | (1,498) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (296) | (300) | (296) | (268) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (1,659) | (1,464) | (1,659) | (1,586) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **1,021** | **586** | **1,021** | **41** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | | - | - |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **1,021** | **586** | **1,021** | **41** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **1,021** | **586** | **1,021** | **41** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 117 | 114 | 117 | 104 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 163 | 93 | 163 | 7 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | 4 | 4 | 4 | 4 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.46% | | 0.46% | 0.03% |
| | (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 4.98% | 0.25% | 4.98% | 0.22% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 59.69% | 2.92% | 59.69% | 82.25% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1.25% | 56.95% | 1.25% | 1.07% |
| | | | 0 | | |

| | *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| 1 | Usman Isiaka<br>**Mkurugenzi Mtendaji** | *Imesainiwa* | *17th April 2020* |
| 2 | Chomete Hussein<br>**Mkuu wa Fedha** | *Imesainiwa* | *17th April 2020* |
| 3 | Joseph Ringa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | *Imesainiwa* | *17th April 2020* |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| | *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| 1 | Amb.Tuvako Manongi<br>**Mkurugenzi** | *Imesainiwa* | *17th April 2020* |
| 2 | Oliver Alawuba<br>**Mkurugenzi** | *Imesainiwa* | *17th April 2020* |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
### KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31-Machi 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka ya sasa 31-Mar-20 | Robo ya Mwaka linganishi 31-Dec-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mar-20 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Mar-19 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | **1,021** | **586** | **1,021** | **41** |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 128 | 434 | 128 | 97 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,722) | (8,204) | (1,722) | 4,492 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (1,953) | (9,007) | (1,953) | (4,195) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (2,225) | 751 | (2,225) | 5,398 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (3,581) | 244 | (3,581) | (246) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 3,486 | 642 | 3,486 | (540) |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| -Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **(4,845)** | **(14,554)** | **(4,845)** | **5,048** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (36) | (343) | (36) | 12 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(36)** | **(343)** | **(36)** | **12** |
| ***III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:*** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (3,510) | (4,038) | (3,510) | 1,647 |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **(3,510)** | **(4,038)** | **(3,510)** | **1,647** |
| IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu: | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(8,390)** | **(18,935)** | **(8,390)** | **6,707** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 116,710 | 135,645 | 116,710 | 25,917 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **108,320** | **116,710** | **108,320** | **32,624** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2020
(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2020** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (40,582) | - | - | - | 19,942 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 1,021 | - | - | - | 1,021 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | | | - | | - | | |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(39,561)** | **-** | **-** | **-** | **20,963** |
| **Mwaka uliopita 2019** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (42,568) | - | 402 | - | 18,358 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 1,668 | - | - | - | 1,668 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | 402 | - | (402) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(40,498)** | **-** | **(0)** | **-** | **20,026** |

United Bank for Africa (T) Ltd is a subsidiary of United Bank for Africa Plc, a leading Pan African bank offering universal banking to more than 13 million customers in over 1000 branches and outlets in Africa , USA and Europe .

**East & South Africa**
- Tanzania
- Kenya
- Congo DRC
- Mozambique
- Uganda
- Zambia

**Central Africa**
- Cameroon
- Gabon
- Tchad
- Congo Brazzaville

**West Africa**
- Ghana,
- Benin
- Burkina Faso,
- Cote D'Ivoire (CDI)
- Liberia
- Sierra Leone
- Senegal
- Mali
- Guinea

**Europe**
- UK
- France

**USA**
- New York

## HABARI KITAIFA

# Polisi yashikilia watatu madai ya mauaji

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma, linawashikilia watu watatu kwa madai ya mauaji ya mwendesha bodaboda, Patrick Denis (24) kwa kumpiga na kitu kizito kichwani na kumpora pikipiki.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema mauaji hayo yalitokea Aprili 15, maeneo ya Area C, Kata ya Mlimwa, jijini hapa.

Alisema baada ya Jeshi la Polisi kufanya msako ilimkamata Ally Mohamed Musa (22), ambaye ni dereva wa boda mkazi wa Hazina, jijini hapa.

Kamanda Muroto (pichani) alisema katika uchunguzi wao wa awali imefahamika mtuhumiwa kwa muda mrefu amekuwa akifanya uhalifu huo wa unyang'anyaji wa pikipiki kwa kutumia nguvu.

Alisema pikipiki imepatikana na mtuhumiwa anatarajiwa kufikishwa mahakamani kwa kosa la mauaji.

Katika hatua nyingine mtuhumiwa Abdul Ayubu (20), mkazi wa Mnarani, Wilaya ya Kondoa, mkoani hapa, amekutwa na jumla ya pikipiki tisa kati ya hizo sita hazina namba za usajili, kadi za pikipiki 21, vibao vya namba za usajili wa pikipiki tano, na stika za bima nakala nane zilizobanduliwa kwenye pikipiki hizo.


Kamanda Muroto alisema mtuhumiwa ni mpokeaji wa mali za wizi na pikipiki zinazoibiwa kutoka maeneo mbalimbali ndani ya Mkoa wa Dodoma na nje ya mkoa huo.

Alisema baada ya kuzipokea huziingiza kwenye biashara ya dodaboda na nyingine kuuza kwa wakulima.

Kamanda Muroto, aliwataka vijana kufanya kazi za halali ili kuepuka kukamatwa na kusababisha misongamano katika mahabusu za polisi.

Alisema Jeshi hilo litaendelea na msako licha ya kuwapo kwa ugonjwa wa corona, lakini ataendelea kuwalinda wananchi wake na uhalifu unaojitokeza kila kukicha.

Hata hivyo aliwataka wananchi kujikinga na corona ikiwamo kufuata sheria za afya zilizowekwa ili kujikinga na ugonjwa huo kama takwimu zilivyotolewa na Wizara ya Afya.



## Washtakiwa kutoa lugha hatarishi kuhusu corona

**Na Hellen Mwango**

WAKAZI wawili wa jijini Dar es Salaam akiwamo mfanyabiashara Boniface Mwita (49) na Rosemary Jenera (41), wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kujibu tuhuma za kutoa lugha hatarishi kwa jamii kuhusu corona.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Vick Mwaikambo.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mkunde Mshanga na Wankyo Simon, ulidai kuwa washtakiwa hao wanakabiliwa shitaka la kutoa lugha hatarishi au yenye kushawishi jamii.

Ilidaiwa kuwa Machi 20, mwaka huu jijini Dar es Salaam, washtakiwa wakiwa kwenye daladala wakitoka Tabata kwenda Muhimbili, walitoa matamshi hatarishi kwamba, 'ugonjwa wa corona serikali inadanganya, hakuna ugonjwa wowote na imefunga shule kwa kuwa haina pesa na ada za kusomesha watoto bure', walinukuliwa washtakiwa.

Hata hivyo, washtakiwa walikana mashtaka yao.

Wankyo alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika, Jamhuri haina pingamizi la dhamana na aliomba mahakama kupanga tarehe ya kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Mwaikambo aliwataka washtakiwa kuwa na wadhamini wawili wenye barua na vitambulisho na watatia saini hati ya dhamana ya Sh. milioni tano.

Washtakiwa wote walitimiza masharti hayo wako nje kwa dhamana kesi itatajwa Mei 6, mwaka huu.


UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES

| S/N | ITEM/TRANSACTION | | |
|---|---|---|---|
| SECTION A | SAVINGS ACCOUNTS | RETAIL | CORPORATE |
| 1 | FREEDOM SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 5,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 2,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | NIL | |
| 2 | GENERAL SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 | |
| 3 | EMPLOYEE SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS15,000 USD 15 | |
| | Minimum operating balance | TZS 2,000 USD 10 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Adhoc statement request | TZS 1,000/ PAGE | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 4 | SAVINGS ACCOUNT INDIVIDUALS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | 15,000 | |
| | Minimum operating balance | 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 5 | SAVINGS ACCOUNT SALARY | | N/A |
| | Required minimum opening balance | 15,000 | |
| | Minimum operating balance | 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 6 | SAVINGS ACCOUNT DOMICILARY | | |
| | Required minimum opening balance | USD10 | |
| | Minimum operating balance | USD 5 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | 1% per Transaction | |
| | Closing account | USD 5 | |
| 7 | U-CARE CHILDREN SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 USD 15 | |
| | Minimum operating balance | TZS 20,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 | |
| SECTION B | CURRENT ACCOUNTS | | |
| 1 | INDIVIDUAL CURRENT ACCOUNT | | BUSINESS CURRENT ACCOUNT |
| | Required minimum opening balance | TZS 30,000 | TZS 100,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 10,000 | TZS 100,000 |
| | Monthly maintenence fee | TZS 10,000 | TZS 12,000 |
| | Cash withdrawal at counter | 1 PER MILLE | TZS A/C 1 PER MILLE |
| | Closing account | TZS 10,000 | TZS 10,000 |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 10% | TZS A/C PLR + 10% |
| 2 | DIPLOMAT ACCOUNTS | | |
| | Required minimum opening balance | USD 200 | N/A |
| | Minimum operating balance | USD 100 | N/A |
| | Monthly maintenence fee | NIL | N/A |
| | Cash withdrawal at counter | NIL | N/A |
| | Closing account | NIL | N/A |
| | Penalty for overdrawn account | NIL | N/A |
| | Outward fund transfers(TTs) | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 200 | N/A |
| | Inward fund transfers(TTs Incoming) | NIL | N/A |
| | FOREX exchange | Favourable rates will be applied | N/A |
| 3 | DOMICILIARY CURRENT ACCOUNT | | |
| | Required minimum opening balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Minimum operating balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Monthly maintenence fee | USD 12 or its equivalent | USD 15 or its equivalent |
| | Minimum search fees | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 |
| | Cash withdrawal | 1% per Transaction | 1% per Transaction |
| | Cheque book - 25 LEAF | USD 10 or its equivalent | N/A |
| | Closing account | USD 10 | USD 10 |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 2% | PLR + 2% |
| | Transfer From TZS to DOMICILIARY/ DOMICILIARYto TZS | NIL | NIL |
| SECTION C | DEPOSIT ACCOUNTS | | |
| 1 | Call Accounts | | Call Accounts |
| | Minimum opening balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Monthly Average balance requirement | Negotiable | Negotiable |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| 2 | Term Deposits | | Term Deposits |
| | Minimum deposit - local currency | TZS 500,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum deposit - USD | USD 1,000 | USD 10,000 or equivalent |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| SECTION D | ELECTRONIC BANKING | | |
| 1 | E-Banking | | E-Banking |
| | Internet banking monthly subscription | TZS 2,000 Per Month. | TZS 10,000 per Month |
| | Internet banking ( Re issue pin) | TZS 5000 | TZS 5000 |
| | U - Direct (Reversal of transaction) | TZS 4000 | TZS 4000 |
| | E-statement (self downloaded) | FREE | FREE |
| | POS purchase (Local) | FREE | N/A |
| | POS purchase (International) | TZS 6000 (up to 1000$) TZS 10,000 ($1001 - $2000) TZS 20,000 (Above $ 2000) | N/A |
| | ATM reversal | TZS 1,000 per transaction | N/A |
| | Fund transfer/ company load | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | Card Load | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | Manual pin change | TZS 1,500 per transaction | TZS 1,500 per transaction |
| | U-MOBILE(mobile banking-Bank to wallet) | TZS 1,000 (0 - 200,000/=) and TZS 2,000 (200,001 - 400,000/=) | N/A |
| | Card to card transfer | TZS 1,500 per transaction | TZS 1,500 per tr |
| | Africash | TZS 6000 + 1.5% of the amount sent/USD 4.45 + 1.5% | N/A |
| 2 | Visa Debit Card | | N/A |
| | Issuance fees | TZS 10,000 | |
| | Re-issuance fee | TZS 10,000 | |
| 3 | Visa Perapid Cards | | N/A |
| | Issuance fees for instant card | TZS 12,000 | |
| | Issuance fees for personalized card | TZS 16,000 | |
| | Re-issuance fees | TZS 12,000 | |
| | Online Passcode reset fee | TZS 1,500 | |
| | ATM Pin reset fee | TZS 1,500 | |
| | Loading fee | TZS 1,000 | |
| | Online shopping fee - Local transactions | FREE | N/A |
| | Online shopping fee/Web - Int. transactions | TZS 6000 (up to 1000$) TZS 10,000 ($1001 - $2000) TZS 20,000 (Above $ 2000) | N/A |
| 4 | ATM Withdrawals | | N/A |
| | At UBA ATMs (On us) | TZS 500 | |
| | ATM Balance inquiry(Local) | TZS 200 | |
| | ATM Balance inquiry(international) | TZS 1000 | |
| | To other banks ATM (On others/OFF US)Local | TZS 2,500 | |
| | international ATM withdraw | TZS 6000 | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| SECTION E | ASSET BANKING | | |
| 1 | LOANS | | |
| | Processing fee | negotiable | 2% |
| | Insurance for personal loans | N/A | 1.50% |
| | Legal fees | 0.5% minimum of TZS 300,000 | 0.5% minimum of TZS 300,000 |
| 2 | TEMPORARY OVERDAFT (TODs) | | |
| | Processing fee | 2% | 2% |
| SECTION F | TRADE FINANCE | | |
| 1 | Guarantees | | Guarantees |
| | Facility Commission | 2% p.a (0.5% per qtr). Min USD 250 per qrt. | 2% p.a (0.5% per qtr). Min USD 250 per qtr. |
| | Arrangement fees | 2% | 2% |
| | Cash Covered | 0.5% per qtr Min 250 per qtr | 0.5% per qtr Min 250 per qtr |
| | Amendment | USD 100.00 flat | USD 100.00 flat |
| | Extension to next quarter | 0.5% per qtr ( Or % of the agreed rate) | 0.5% per qtr ( Or % of the agreed rate) |
| | Amount increase | 0.5% /qtr on the diff ( Or % of the agreed rate) | 0.5% /qtr on the diff ( Or % of the agreed rate) |
| 2 | Letters of Credit - Imports | | Letters of Credit - Imports |
| | Issuance commision | 0.5% per quarter. Min USD 150. | 0.5% per quarter. Min USD 150. |
| | Handling Fees | USD 100 flat | USD 100 flat |
| | Swift charge | USD 50 flat | USD 50 flat |
| | Amendment | USD 100.00 flat | USD 100.00 flat |
| 3 | Letters of Credit - Exports | | Letters of Credit - Exports |
| | LC Advising Commission | USD 200 flat | USD 200 flat |
| | Amendment advising commision | USD 100 Flat | USD 100 Flat |
| | Correspondences Swift charge | USD 50 flat | USD 50 flat |
| | Documents handling and examination fee | 1.5% of invoice amount ,min usd 200 | 1.5% of invoice amount ,min usd 200 |
| | Courier charge | USD 100 flat | USD 100 flat |
| | LC confirmation charges | 1.5% per quarter (only for confirmed usance lcs) | 1.5% per quarter (only for confirmed usance lcs) |
| 4 | Letters of Credit Refinancing | | Letters of Credit Refinancing |
| | Interest on refinance | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 |
| | Commission on refinance | USD 50 flat | USD 50 flat |
| 5 | Discounting on LC/Invoice/Cheque | | |
| | Interest on discounting | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 |
| | Commission on discounting | USD 50 flat | USD 50 flat |
| 6 | Bills Discounting (Bills of exchange including cheques) | | |
| | Interest on discounting | PLR +3%-local; International Lobor+8% | PLR +3%-local; International Lobor+8% |
| 7 | Documentary Collection - Export | | |
| | Handling charge | 0.25% of the invoice min USD 100 flat | 0.25% of the invoice min USD 100 flat |
| | Courier charge | USD 100 | USD 100 |
| | Corespondence commission | USD 50 Per tracer | USD 50 Per tracer |
| 8 | Documentary Collection - Import | | |
| | Handling Commission | 0.25%. Min USD 100 | 0.25%. Min USD 100 |
| | correspondence Swift charge | USD 50 | USD 50 |
| 9 | Outward Bills for Collection (clean collections & TCs) | | |
| | Handling Commision | 0.25% of value, min USD 75 or its equivalent | 0.25% of value, min USD 75 or its equivalent |
| | Dhl charges | usd 75 flat | usd 75 flat |
| | Returned foreign cheques | claimed charges + locally un re-covered charges | claimed charges + locally un re-covered charges |
| 10 | Inward Bills for Collection | | |
| | Handling Commission | USD 50 flat per collection | USD 50 flat per collection |
| | Swift charged | USD 40 flat per collection | USD 40 flat per collection |
| 11 | Local Currency Transactions | | Local Currency Transactions |
| | Outward remittances (TISS) | TZS10,000 PER TRANSACTION | TZS10,000 PER TRANSACTION |
| | Amendment fee for Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers by customer or by bank | TZS 10,000.00 OR ITS EQUIVALENT | TZS 10,000.00 OR ITS EQUIVALENT |
| | Inward Swift Transfers (TISS) | NIL | NIL |
| 12 | Foreign Currency Transactions | | Foreign Currency Transactions |
| | Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 500 | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 500 |
| | Telegraphic Overseas Charges/ OURS | USD/EUR/GBP 35 FLAT (OURS) | USD/EUR/GBP 35 FLAT (OURS) |
| | Amendment fee for Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers by customer or by bank | USD 10 FLAT | USD 10 FLAT |
| | Inward Swift Transfers | USD 10 FLAT | USD 10 FLAT |
| | International Money Order (IMO) | USD 30 per IMO | USD 30 per IMO |
| | Foreign cheques for collection | 0.25% of value. USD 75 min; USD 250 max; | 0.25% of value. USD 75 min; USD 250 max; |
| SECTION G | OTHERS | | |
| 1 | Statements | | Statements |
| | Monthly | FREE | FREE |
| | Adhoc requests | TZS 1,000/ PAGE | TZS 1,000/ PAGE |
| 2 | Cheque Books Issuing | | Cheque Books Issuing |
| | - 25 Leaf | TZS 15,000; USD 10 | N/A |
| | - 50 Leaf | TZS 30,000; USD 20 | N/A |
| | - 100 Leaf | TZS 45,000; USD 30 | TZS 45,000; USD 30 |
| | Counter cheque request | TZS 20,000; USD 10 | TZS 20,000; USD 10 |
| | Cheque Stop payment instructions | leaf lost: TZS 20,000; Book lost: TZS 40,000; | Leaf lost: TZS 20,000; Book lost: TZS 40,000; |
| | Issuance of Manager's cheque | TZS 25,000; USD 20 per item | TZS 25,000; USD 20 per item |
| | Managers cheque cancellation charges | FREE | FREE |
| 3 | Standing order | | Standing order |
| | Standing order set-up | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent |
| | Standing order maintanance | NIL | NIL |
| | Standing order/Foreign Bank (TT charge) | MIN USD 50; 0.25% MAX USD 500 | MIN USD 50; 0.25% MAX USD 500 |
| | Amend / Stop standing Order | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent |
| | Unpaid standing order | TZS 40,000; USD 40 or its equivalent | TZS 40,000; USD 40 or its equivalent |
| 4 | Insufficient funds/effects not cleared | | Insufficient funds/effects not cleared |
| | Effects not cleared | **ITEM REMOVED** | **ITEM REMOVED** |
| | Insufficient Funds (Refer to drawer) | TZS 50,000; USD 50 | TZS 50,000; USD 50 |
| 5 | Other services/charges | | |
| | Retriving old documents (2-6 months) | TZS 10,000; USD 10 | TZS 10,000; USD 10 |
| | Retriving documents (6 months and above) | TZS 15,000; USD 15 | TZS 5,000; USD 15 |
| | Confirmation/Audit/ Certificate of balance | TZS 50,0,000; USD 25 or its equivalent | TZS 50,0,000; USD 25 or its equivalent |
| | Status enquiry / Reference Letters | TZS 25,000; USD 25 or its equivalent per customer request | TZS 25,000; USD 25 or its equivalent |
| | Manual processing of salaries | TZS 1,000; USD1 or its equivalent | TZS 1,000; USD1 or its equivalent |
| | Closure of Account | TZS10,000 | TZS10,000 |
| | Dormant Account Reactivation | FREE | FREE |
| | Cash handling fee-COINS ONLY | 9% of the Deposit | 9% of the Deposit |
| 6 | Soiled notes | 3% of principal amount | 3% of principal amount |
| 7 | Coins | 3% of principal amount | 3% of principal amount |
| | | | |
| | **approved by:** | | |
| | **Signature:** | | **Signature:** |
| | | | |
| | Flavia Kiyanga | | Chomete Hussein |
| | **Chief Operating Officer** | | **Country Chief Finance Officer** |
| | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** | | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** |
| | **Disclaimer: All fees are VAT exclusive.** | | |

United Bank for Africa (T) Ltd is a subsidiary of United Bank for Africa Plc, a leading Pan African bank offering universal banking to more than 13 million customers in over 1000 branches and outlets in Africa , USA and Europe .

**East & South Africa**
- Tanzania
- Kenya
- Congo DRC
- Mozambique
- Uganda
- Zambia

**Central Africa**
- Cameroon
- Gabon
- Tchad
- Congo Brazzaville

**West Africa**
- Ghana,
- Benin
- Burkina Faso,
- Cote D'Ivoire (CDI)
- Liberia
- Sierra Leone
- Senegal
- Mali
- Guinea

**Europe**
- UK
- France

**USA**
- New York

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kuruhusu ulaji huu ni kuchezea corona

**UUZAJI** wa chakula mitaani kwenye miji midogo, mikubwa na majiji nchini ni ujasiriamali unaokubalika. Tena, kazi hii ya baba na mamalishe inachukuliwa kama huduma muhimu ya kuwapa wananchi chakula kwa gharama nafuu wanazozimudu.

Lakini, kutokana na maradhi yanayoibuka sasa ya corona nilazima kubadilika kwa kuwa kuendeleza mitindo ya maisha kimazoea, watu wanaweza kuambukizwa maradhi kupitia kula vyakula vya baba na mamalishe.

Tunasema hivi kwa sababu kwa sekta hii hakuna anayeifuatilia na pengine huendeshwa bila kufuata sheria na huko ndiko kwenye mwanya wa kusambaza maradhi hasa wakati huu wa corona. Kwanza vyakula huuzwa popote, hakuna majisafi, maliwato wala kantini safi za kukaa na kula.

Tunaona kuwa ulaji vyakula kama mahindi ya kuchoma, kuchemsha, matunda, miwa, ugali, wali na vitafunio magengeni pamoja na pweza pembeni ya barabara si afya ni kuongeza riski za kiusalama na kiafya kwa kusambaza magonjwa mengi ikiwamo corona. Tunaona kuwa Tanzania hatujawa makini kwenye suala la kuzuia kuuza vyakula mitaani na kulipiga marufuku kwa vile kinaweza kuwa chanzo kikuu cha kusambaza maradhi ya corona ambayo yameenea nchi nzima.

Tunaposema ni lazima kuzingatia usafi na kujitakasa tunamaanisha kuwa mikakati ya kunawa mikono, kutumia vitakasa mikono, kula chakula kisafi na kujiepusha na kutumia vitu vyenye hofu ya maambukizi kama vyakula ikomeshe mambo hayo.

Kula miwa inayochongwa hata bila kunawa mikono na kujazwa kwenye mifuko ya nailoni ambayo nayo si salama nako kuinaweka jamii kwenye hatari ya kupata maambukizi.

Kula pweza na ngizi kwa kutumia vijiti vya kusafisha meno tena kwa kuchovya ndani ya chombo kimoja cha pilipili, huku walaji wakiwa wamesongana tena bila kutakasa mikono ni kama kuruhusu watu wetu waambukizwe.

Tunaiomba serikali ifikirie mara moja kupiga marufuku kuchoma mahindi, kula pweza, vyakula magengeni, miwa, kunywa juisi za kutengeneza na kujazwa kwenye chupa zinazookotwa majalalani, kula karanga, tambi na kila aina ya vyakula vinavyopatikana kwenye vituo vya mabasi na popote pale mijini na majijini.

Tunashauri kuwa kutumia kinga na tahadhari ni muhimu kwani virusi vya COVID-19 huambukizwa kutokana na kutozingatia usafi na kutonawa mara kwa mara pamoja na kutumia mikono isiyotakaswa kushika na kula vitu ambavyo havijatakaswa. Hili ni muhimu kulizingatia kwa kuwa ugonjwa huu wa corona ni kama taifa lipo vitani. Bila kuzingatia usafi na maelekezo ya watalaamu tunaweza kujikuta katika hali mbaya na idadi kubwa ya watu ikiaathirika.

Tunaona kuwa tunapokuwa vitani kuna haja ya kufuata maelekezo ya watalaamu na kujitahidi kuwalinda watu wetu kwa vile wanaoumia ni Watanzania na gharama kubwa ya matibabu itabebwa na taifa na kuwa katika hali ngumu zaidi ya kuhudumia wagonjwa pengine ambao wanaweza kuwa mzigo usiobebeka.

Tukumbuke kukinga ni tiba kuliko kutibu wagonjwa wa maradhi haya ambayo ni kitisho kwa wananchi wetu kwa vile wengi hawana uelewa na elimu ya kutosha kuhusu maradhi haya.

Tunashauri tahadhari hii ichukuliwe mapema kama ambavyo viongozi wanasisitiza uvaaji barakoa vivyo hivyo wahimize watu kuacha kuuza vyakula na kula chakula mitaani ambacho inawezekani kimechafuliwa na corona.

Lakini si hivyo tu, pia kuwahimiza watu wasijikusanye kwenye mikusanyiko magengeni kula vyakula kwa mama na babalishe jambo linaloweza kuwa na athari kwenye afya zao.

Tunaomba serikali isipuuze izingatie masuala haya ya kula ovyo mitaani ili kudhibiti njia zinazoweza kusababisha ugonjwa kusambaa kwa kasi kubwa, zaidi, ikizingatiwa kuwa ni kama umefika mikoa yote ya Bara na Visiwani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kung'atuka ndio kulinda heshima

**WAKATI** vikao vya bunge vinaendelea jijini Dodoma, baadhi ya wabunge wameanza kuaga rasmi wakisema kwamba hawatajitosa kwenye kinyang'anyiro katika uchaguzi mkuu ujao.

Wabunge hao ni kutoka majimbo ya mkoa wa Kagera, Wilfred Lwekatare wa Bukoba Mjini (Chadema), Profesa Anna Tibaijuka wa Mulema Kusini (CCM) na pia yupo wa kuteuliwa, Abdallah Bulembo.

Kikubwa ambacho wanakisema, ni kwamba wameamua kustaafu au kung'atika ili kupokezana vijiti na wengine, kwa vile nafasi hizo ni za kuachiana na siyo mali ya mtu mmoja.

Kimsingi walichofanya kinalingana na hali ya sasa kwamba, mtu anaongoza akitambua umuhimu wa kupokezana vijiti badala ya kudhani kuwa nafasi hiyo ni yake tu hatakiwi mtu mwingine kuiwania.

Hayo yalikuwepo enzi hizo, lakini sasa mambo yamebadilika, kwa sababu mwanachama anapingwa kuanzia ndani ya chama chake hadi nje, kwa hiyo akisoma ishara za nyakati ataongeza na kisha kuachia wengine.

Sina maana kwamba hao waliotangaza kung'atuka hawatakiwi, hapana, bali hatua yao inaonyesha ni jinsi gani wanatambua umuhimu wa kuongoza na kisha kuwaachia wengine wachukue nafasi.

Miaka ya nyuma kulikuwa na wabunge ambao walishikilia nafasi hiyo kwa miaka 40 hadi walipoamua kwa hiyari yao wenyewe kustaafu, lakini sasa hali sivyo kabisa, kwani upinzani umekuwa ni mkali.

Upinzani ni mkali unaanzia ndani ya chama, hivyo wale wasiotaka kung'atuka ili kuwaachia wengine wawanie ubunge, wajue kuwa wanakabiliwa na upinzani ambao wakati mwingine unaweza wakapotea katika siasa.

Ikumbukwe kuwa, siku hizi kumekuwa na uwazi kutokana na wingi wa vyombo vya habari, Watanzania wanajua kinachofanyika bungeni, hivyo kama mbunge wao hana mchango wowote inakuwa rahisi kujua.

Mbaya zaidi ni kwamba kama wamemchoka, huwa wanasema wazi, hivyo suala la kusoma ishara za nyakati ni la msingi sana ili kama mbunge akigundua kuwa wapigakura wamemchoka, basi asijitose tena katika kinyang'anyiro.

Tofauti na miaka ya zamani, vijana ambao pia ni wasomi wanazidi kujitokeza kwenye siasa wakitafuta nafasi mbalimbali za uongozi na wanaweza kuwaangusha wakongwe, hivyo siyo vibaya wakongwe wakawapisha.

Katika maelezo yake akitangaza kung'atuka, Prof. Tibaijuka, aliwahi kusema kwamba anawapisha vijana wenye mawazo mapya ili washike nafasi hiyo huku yeye akiwa nyuma yao kuwasimamia na kuwashauri.

Badala ya kuwa na kinyongo, mbunge anaweza kuongoza kisha akastaafu, halafu uzoefu wake wa kukaa bungeni ukatumiwa na mrithi wake kusaidia kufikia maendeleo ambayo jimbo limejiwekea.

Wabunge hao kwa hiyari yao, wametangaza kustaafu, hivyo matarajio ni kwamba wale watakaochukua nafasi wanaweza kuwatumia kupata uzoefu kufanya shughuli za maendeleo majimboni mwao.

Kwa upande wake Prof. Tibaijuka ameshaweka wazi kuwa anamalizia muda wake wa ubunge uliobakia, kisha akae pembeni na kuwaachia vijana ili awe nyuma yao akisaidia kuwashauri.

Lakini pia hatua hii inaweza kusaidia kumfanya mbunge aondoke akiwa bado anapendwa na wapigakuta wake kuliko kuchokwa na kuanza kuzomewa kama ambavyo imewahi kutokea kwa wale wanaong'ang'ania madaraka.

Hili nalo ameliona mbunge wa Rorya mkoani Mara, Lameck Airo (CCM) ambaye amewahi kuliambia gazeti hili kuwa mwaka huu hatawania tena ubunge akidai kwamba anataka astaafu wakati bado wananchi wakimpenda.

Huu ni uamuzi mzuri, kwani wapigakura wakimchoka mtu mwisho wake ni aibu, hivyo suala la kusoma ishara za nyakati ni la msingi kuliko kung'ang'ania kana kwamba hakuna watu wengine wanaoweza kuongoza jimbo.

Mbunge huyo amewahi kurudia mara kadhaa kauli yake ya kung'atuka ingawa bado hajaaga bungeni kama wenzake walivyofanya, hata hivyo, ukimya huo hauwezi kumaanisha kuwa amebadili gia angani.

Bunge hili ndilo la mwisho kabla ya kuvunjwa na huenda akaaga au wakajitokeza wabunge wengine zaidi ambao ni wakongwe wakaamua kuaga baada ya kutumikia majimbo kwa muda mrefu.

Lakini pia sina maana kwamba kuongoza majimbo kwa muda mrefu ni kigezo ya kutochaguliwa, bali jambo la msingi ni kutambua uongozi ni kupokezana kwa kutumia mtindo wa kung'atuka.

HABARI KITAIFA

# Jengo la kuhifadhi kinga za corona laungua moto

**"Jengo hili liloungua ni jengo la stoo ambalo linahifadhi vitu tofauti tofauti, zikiwamo na kemikali mbalimbali na hasa chloride na kemikali nyingine nyingine ambazo zilikuwa zinatumika kwa ajili ya 'ku-sanitize' (kutakasa) na pia kwa ajili ya kuua wadudu na vitu vingine vya kufukiza," alisema.**

**Na Enock Charles**

JENGO la kuhifadhia dawa za kujikinga na maambukizo ya corona lililoko Temeke jijini Dar es Salaam, limeteketea kwa moto na kuunguza aina mbalimbali za dawa zilizokuwa zimehifadhiwa.

Akizungumza katika eneo la tukio jana, Kamanda Msaidizi wa Jeshi la Zimamoto Mkoa wa Temeke, Bakari Mrisho, alisema jengo hilo lilikuwa limehifadhi kemikali zilizokuwa zikitumika kusafisha maeneo kwa ajili ya kuua wadudu.

"Jengo hili liloungua ni jengo la stoo ambalo linahifadhi vitu tofauti tofauti, zikiwamo na kemikali mbalimbali na hasa chloride na kemikali nyingine nyingine ambazo zilikuwa zinatumika kwa ajili ya 'ku-sanitize' (kutakasa) na pia kwa ajili ya kuua wadudu na vitu vingine vya kufukiza," alisema.

Kamanda Mrisho alisema moto huo uliwaka kwa takriban saa nzima hadi pale walipofanikiwa kuuzima na kuokoa majengo mengine matatu kuwaka, ingawa bado haijafahamika chanzo chake.

## Afariki dunia basi, lori yakigongana

**Na Elisante John,** SINGIDA

MTU mmoja amefariki dunia na wengine saba kujeruhiwa baada ya basi lililokuwa likitoka Morogoro kwenda Mwanza kugongana na lori la mizigo. Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Sweetbert Njewike, alisema ajali hiyo ilitokea juzi saa moja usiku katika Kijiji cha Unyahati, wilayani Ikungi, na kumtaja marehemu kuwa ni kondakta wa basi hilo Selemani Said (35), mkazi wa Morogoro.

Alisema, chanzo cha ajali ni mwendo kasi wa dereva wa basi aliyekuwa anajaribu kulipita lori la mizigo bila ya kuchukua tahadhari na kugongana uso kwa uso na lori lingine lililokuwa linakuja mbele, baadaye magari yote mawili kuwaka moto.

Aliwataja majeruhi wa ajali hiyo kuwa ni Mayala Elikana (20) na Silinge Lazaro (27), wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) cha Morogoro, Thomas Michael (60), Safania Ibrahimu (57) na Yusufu Nyatari (26), wote wakazi wa jijini Dar es Salaam, pamoja na Ruth Simon (16) Haji Abeid (25), wote wakazi wa Mwanza.

Kamanda Njewike alisema majeruhi wote wanaendelea na matibabu katika hospitali ya Mission Puma, Wilaya ya Ikungi na wanaendelea kumtafuta dereva wa basi Goodluck Masatu, aliyekimbia baada ya ajali.

Kutokana na ajali hiyo, Jeshi la Polisi, Mkoa wa Singida limeendelea kuwakumbusha watumiaji wote wa barabara kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepusha ajali zisizokuwa za lazima.



HABARI KITAIFA

# Kemikali iliyotaifishwa kutengeneza vitakasa mikono

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imetoa kemikali aina ya 'Ethyl Alcohol' mapipa 367 yenye lita 91,976 yaliyokamatwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya kulevya Desemba, mwaka 2017 yaliyoingizwa nchini na kutaifishwa na serikali.

Akizungumza wakati akikabidhi kemikali hizo kwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, Kamishna wa Mamlaka hiyo, James Kaji, alisema baada ya kukamatwa kemikali hizo zilipelekwa mahakamani na hukumu iliamuru kemikali hizo kutaifishwa na serikali itumie kutengeneza vitakasa mikono vitakavyouzwa kwa bei nafuu ili kudhibiti na kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19, ili kila Mtanzania aweze kujikinga.

Alisema kutokana na mkoa huo kuwa na maambukizi yanayoendelea na juhudi za Mkuu wa mkoa huo kuhakikisha wananchi wake wanafuata maelekezo ya wataalamu wa afya, ndio chanzo cha serikali kukubali wazo la kutengeneza vitakasa mikono kwa kutumia kumikali hiyo.

"Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Ofisi ya Kanda ya Ziwa ilitoa ushauri kuwa kemikali hizo ziuzwe na serikali kupata mapato au kutengeneza vitakasa mikono ambavyo vitauzwa na serikali kupata pesa, lakini pia itasaidia kupambana na maradhi ya corona hivyo ushauri wa kutengeneza vitakasa mikono ulikuwa na tija licha ya serikali kupata fedha ulizingatia mahitaji ya wakati huu tulionao kwa taifa letu hasa mlipuko wa janga la corona," alisema Kaji.

Naye Bonaventure Masambu, Meneja wa Kanda, alisema baada ya kukabidhiwa kemikali hiyo ilifanyiwa uchunguzi na kubaini kuwa na ubora kati ya asilimia 89.0 hadi 94 na kulingana na viwango vya Shirika la Afya Duniani (WHO) kitakasa mikono kinahitaji kuwa na asilimia 60 hadi 79 huku kiwango pendekeza kikiwa ni asilimia 70.

Alisema watasimamia kwa uadilifu na weledi kazi hiyo na kuhakikisha kamikali hizo hazirudi sokoni.




Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Musa Kilakala (kushoto), akikabidhi tangi la maji kwa Ofisa wa Afya Soko la Samaki Feri, Mery Mkwazi, kwa ajili ya kunawa mikono kwa wananchi wanaotumia soko hilo, jana. Katikati ni Mwenyekiti wa CCM Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# DC ataka Vicoba kuendeshwa kimtandao

**Na Edina Alex, SINGIDA**

MKUU wa Wilaya ya Singida, Mhandisi Paskas Mulagiri, amewataka wanawake wanaojishughulisha na Vicoba kufanya shughuli hizo kwa njia ya mtandao ili kujiepusha na maambukizi ya corona.

Alisema hayo wakati akifungua Mkutano Mkuu wa Chama cha Walimu (CWT), Manispaa ya Singida.

"Ninyi walimu wanawake ni watu muhimu sana katika jambo hili la corona, ambalo limeikumba taifa letu na dunia kwa ujumla kwa kutoa elimu kwa jamii jinsi ya kujikinga na ugonjwa huu," alisema Mulagiri.

Alisema wanawake wanaofanya shughuli za Vicoba wanapaswa kutumia njia ya mtandao ili kujiepusha na msongamano.

Pia alisema, bila kuwa makini katika suala hilo na ikatokea mmoja wao kupata maambukizi hali itakuwa mbaya zaidi.

Kadhalika, alisema kundi la walimu likiamua kutoa elimu kwa nguvu ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, mafanikio yatakuwa makubwa katokana na jamii kuwaamini.

Alitoa wito kwa wananchi wa Manispaa ya Singida kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya na serikali jinsi ya kujikinga na ugonjwa huo.

# Wateja Tigo warahisishiwa huduma za fedha

**Na Enock Charles**

WATUMIAJI wa huduma za simu za mkononi wa Kampuni ya Tigo, wamewezeshwa kwa kurahisishiwa utumaji na upokeaji wa fedha.

Uwezeshaji huo umetokana na kampuni hiyo kuzindua huduma inayowawezesha watumiaji wote wa Tigo Pesa nchini kutuma na kupokea pesa kupitia simu zao za mkononi kutoka M-PESA ya Kenya, MTN nchini Uganda, Airtel na MTN za nchini Rwanda.

Huduma hiyo imeelezwa kuwa ni ya wazi na inawaunganisha wateja wa Tigo Pesa na mitandao mingine mikubwa ya mawasiliano katika ukanda wa Afrika Mashariki, inayotoa huduma za kifedha kupitia simu za mkononi.

Hatua hiyo imetajwa kuwa itakuza wigo wa kufanya miamala ya kifedha bila kujali mipaka baina ya nchi moja na nyingine.

Taarifa ya Kaimu Ofisa Mkuu wa Huduma za Kifedha wa Tigo Tanzania, Angelica Pesha, kwa vyombo vya habari, alisema kuwa huduma hiyo mpya baina ya nchi nne inadhihirisha namna Tigo ilivyojizatiti kwenda sambamba na mahitaji ya wateja wake kwa kutua suluhu ya kidigitali.

" Ushirikiano huu unaifanya kampuni yetu kuwa chaguo la wengi katika masuala ya huduma za kifedha na tunaamini kwamba hatua hii mpya itaweza kukuza miamala ya kifedha pamoja na biashara katika mataifa yote manne," alisema Pesha.

Alisema kuimarishwa kwa umoja baina ya Safaricom, MTN, Airtel na Tigo Tanzania, utawezesha kufikia mahitaji ya kufanikisha miamala ya kifedha ndani ya Afrika Mashariki. M-PESA imekuwa huduma inayokubalika na Wakenya wengi kimataifa ambao wamekuwa wakiiona kuwa ya haraka, salama, yenye unafuu na rahisi.

HABARI KITAIFA

## Wakulima kunufaika soko zao la mtama

**Na Sabato Kasika**

WAKULIMA wadogo 1,400 kutoka mikoa ya Dodoma na Manyara, wanatarajia kunufaika na ushirikiano wa mradi wa majaribio wa kununua mtama utakaozalishwa na wakulima hao.

Hiyo inatokana na kampuni ya TBL Plc kukubali kushirikiana na taasisi ya Farm to Market Alliance (FtMA) na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), upande wa Tanzania kuwezesha wakulima wa zao hilo nchini.

TBL Plc kwa kushirikiana na WFP na FtMA, zitawawezesha wakulima wa mtama pia kutafutiwa soko la zao hilo katika mradi huo wa majaribio unaoambatana na TBL Plc kununua mtama utakaozalishwa.

Mkurugenzi Mkuu wa TBL Plc, Philip Redman, alisema jijini Dar es Salaam jana kwamba, mradi huo utafanikisha kuongeza uzalishaji wa mtama nchini na wakulima kunufaika kwa kuwa na kipato cha uhakika.

Alisema, chini ya ushirikiano huo wakulima wa mtama watapatiwa mbegu, bima za mazao, elimu kuhusu kilimo cha mtama, huduma ya wataalamu wa kilimo na jinsi ya kuongeza mavuno na upanuzi wa masoko.

"Tunaamini ushirikiano huu na FtMA na WFP utanufaisha wakulima ambao watapatiwa mbegu bora, huduma ya kutembelewa na wataalamu wa kilimo ili kuwashauri kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mtama," alisema Redman.

Alisema wao wananunua mtama kutoka kwa wakulima wadogo nchini kwa kushirikiana na FtMA na WFP kuimarisha mnyororo wa thamani na kuboresha maisha ya wakulima wadogo ambao ni wazalishaji wakuu.

"Tunatarajia kuanza kutumia programu ya ununuzi inayojulikana kama BanQu ambayo italeta ufanisi na uwazi katika shughuli zetu za manunuzi," alisema.

Alisema, BanQu inawawezesha wakulima kuweka rekodi za miamala na mahesabu yao kidigitali kama uzalishaji, mauzo, ununuzi wa pembejeo pia inawezesha wakulima kulipwa kupitia simu zao za mkononi.

"Hii inawawezesha wakulima kuwa na chakula na kuingia katika mfumo rasmi wa kupata huduma za kifedha na kibenki, kuongeza uzalishaji ambapo TBL Plc kama mnunuzi wa mazao yao itawawezesha kujipatia kipato ili kujikomboa kiuchumi," alisema.

Alisema, mwaka uliopita, TBL ilitumia zaidi ya Sh. bilioni 36.6 kwa ajili ya kununua malighafi kupitia mpango wake wa kununua malighafi ndani na kwamba mchango wao kupitia kununua malighafi za ndani unaenda sambamba na jitihada za serikali za kukuza uchumi wa Tanzania.

Kwa upande wake mwakilishi wa WFP nchini, Michael Dunford, alisema, ukosefu wa soko la uhakika ni kikwazo kinachorudisha nyuma wakulima kuimarisha shughuli zao za kilimo.

# Viwanda Dar kutengeneza barakoa milioni 3.5

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, amesema viwanda viwili vya jijini Dar es Salaam, vimemwahidi kuwa na uwezo wa kutengeneza barakoa milioni 3.5 kwa mwezi.

Aliyasema hayo jana, wakati alipotembelea viwanda vinavyotengeneza barakoa na vitakasa mikono kuangalia maendeleo ya uzalishaji wake kwaajili ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Moja ya kiwanda hicho ni Prestine ambacho kwa sasa kinazalisha barakoa 30,000 kwa siku na baada ya malighafi zake kuingia kutoka nje ya nchi kitakuwa na uwezo wa kuzalisha barakoa 50,000 kwa siku.

Waziri Bashungwa alikitembelea kiwanda hicho na kujionea mahitaji yake hivyo kuwasiliana na Ubalozi wa India, Uturuki na China ili waviingize nchini. Vile vile, Waziri Bashungwa aliwashukuru mabalozi wa nchi hizo hapa nchini kwa kuwa wamesaidia kiwanda hicho kuendelea na uzalishaji na baadhi ya malighafi wanazoendelea kufuatilia kutoka India.

Waziri pia alitembelea kiwanda cha Five Star maeneo ya Vingunguti, jijini Dar es Salaam kinachotarajia kutengeneza barakoa 100,000 kwa siku hali ambayo alisema itasaidia kwa kiasi kikubwa kupambana na ugonjwa huo. "Kwa hiyo ukichukua viwanda viwili kwa muda wa mwezi mmoja hivi vitakuwa vinatengeneza barakoa zisizopungua milioni 3.5 hiyo ni hatua muhimu sana kwa kipindi hiki ambacho Watanzania tunapambana na ugonjwa wa Corona," alisema Waziri.

Lengo la ziara ya Waziri Bashungwa ilikuwa kuangalia uwezo wa uzalishaji wa vifaa hivyo kwa kipindi hiki cha maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona na kuwaagiza wazalishaji wa vifaa hivyo kuboresha zaidi uzalishaji wa vitakasa mikono na barakoa.

Waziri pia aliwataka wazalishaji hao kuangalia jinsi vifaa hivyo vinaweza kuzalishwa kwa wingi nchini ili Watanzania wengi waweze kuvitumia kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo.




Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (wa pili kushoto), akipokea msaada wa ndoo za kunawia mikono kwa sabuni na maji tiririka ambazo zitasambazwa kwenye maeneo ya huduma za jamii kutoka kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira mjini Shinyanga (Shuwasa), Flaviana Kifizi, ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya Corona. Wa kwanza kushoto ni Katibu Tawala la Wilaya ya Shinyanga, Boniphace Chambi na wa kwanza kulia ni Ofisa Uhusiano wa mamlaka hiyo ya maji (Shuwasa), Nsianel Gerald.

# Narco yaagizwa kuweka mipaka kuepusha migogoro

**Na Restuta Damian,**

MULEBA

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Olesante Gabriel, ameitaka Kampuni ya Ranchi ya Taifa (Narco) mkoani Kagera, kuendelea kuweka vigingi vya alama ya mipaka itakayosaidia mwekezaji kutambua mwisho wa mpaka pamoja na wasimamizi kujua eneo alilopangisha.

Alisema hayo katika kikao na timu ya wataalamu wa upimaji wa ardhi inayoshughulikia marekebisho ya ramani ya ranchi mpya ya Mwisa2 inayoshirikiana na uongozi wa wilaya ili kukomboa wafugaji waliokosa maeneo.

Gabriel alisema ranchi ya Mwisa yenye ukubwa wa hekta zaidi ya 133,000 itapunguza migogoro ya muda mrefu baina ya wafugaji na wakulima waliokosa maeneo ya malisho mifugo yao.

Alisema katika nchi kuna jumla ya ranchi 14 kati ya hizo Kagera ina ranchi tano zinazomilikiwa na Narco licha ya wawekezaji kutolipa kodi ya upangaji wa vitalu vinavyopatikana ndani ya ranchi hizo.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Narco, Masele Shilagi, alisema upimaji ulianza mwezi Aprili mwaka huu, kwa kupima maeneo ya eneo hilo.

Alisema lengo kubwa ni kupunguza migogoro ya wafugaji na wawekezaji kwa kukosa maeneo ya kulisha mifugo yao.

Shilagi alisema baada ya shughuli hiyo Narco itapata nafasi nzuri ya kuwapo na ufugaji bora unaotakiwa na kampuni na kumsaidia mwekezaji kunenepesha mifugo yake.

# Mbunge ataka askari wa wanyamapori wabanwe

MBUNGE wa Viti maalum (Chadema), Rhoda Kunchela, (pichani) ameitaka serikali kulieleza Bunge hatua ilizochukua dhidi ya askari wanyamapori waliokiuka sheria na kusababisha madhara makubwa kwa wananchi.

Kunchela alihoji kuhusu suala hilo jana alipouliza swali bungeni, akisema kuwa kumekuwapo na uonevu, mifugo kutaifishwa na kutozwa faini zinazokiuka sheria za nchi.

Pia, alisema kumekuwapo na migogoro ya muda mrefu kati ya hifadhi na wafugaji nchini, hali inayosababisha jamii ya wafugaji kupata madhara mbalimbali ikiwamo vifo.

"Je, serikali inachukua hatua gani kwa baadhi ya askari wanyamapori wanaofanya uonevu huu unaokiuka sheria mbalimbali kwa wafugaji nchini?" alihoji.

Katika majibu yaliyotolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mbunge huyo, ilielezwa kuwa serikali inawatambua wafugaji ambao wamepata madhara.

Wizara hiyo ilisema wafugaji wamekuwa wakiingiza mifugo yao ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa na wamekuwa wakikamatwa na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

"Utaratibu unaotumika kuwakamata wafugaji hao mara zote unazingatia sheria na taratibu zinazosimamia maeneo ya hifadhi, askari wa wanyamapori wamekuwa wakifanya kazi zao kwa kufuata sheria za nchi katika ulinzi wa rasilimali za taifa," ilisema.

Wizara hiyo pia ilisema serikali imekuwa ikitoa msisitizo kwa watumishi kufuata sheria na taratibu kuwakamata wale wote wanaoingiza mifugo ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa ikiwa ni pamoja na kuwafikisha katika vyombo vya sheria.

"Kwa nyakati tofauti kumekuwa na matukio ya wafugaji kuvamia vituo vya askari na kuwashambulia kwa silaha za jadi kwa lengo la kuchukua mifugo yao, suala ambalo ni kinyume cha sheria za nchi,"ilisema.

Ilitolea mfano katika Hifadhi ya Taifa Ruaha ambako Oktoba 9, 2018, askari wanyamapori aliuawa na wananchi waliovamia Kituo cha Nyota kwa lengo la kukomboa mifugo yao iliyokuwa imekamatwa baada ya kuingizwa katika hifadhi hiyo kinyume cha utaratibu.

"Katika hifadhi hiyohiyo, tarehe 03/07/2016, askari mwingine wa wanyamapori aliuawa na wananchi waliovamia kituo cha Ikoga kwa lengo la kukomboa mifugo yao," ilisema.



Wizara ilibainisha kuwa askari wa wanyamapori wanaobainika kukiuka sheria, kanuni na taratibu, wizara imekuwa ikiwachukulia hatua stahiki za kinidhamu kulingana na sheria, kanuni na taratibu za kiutumishi.


Ilisema katika kuendelea kutafuta suluhisho la uingizaji wa mifugo ndani ya hifadhi, serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika maeneo yanayozunguka hifadhi kadri bajeti itakavyokuwa inaruhusu.

# Neema wakulima wa shayiri, ngano

BUNGE limeelezwa kuwa katika kulinda wakulima wa shayiri na ngano nchini, serikali inaandaa mpango wa kupunguza uagizaji wa ngano na shayiri kwa kutumia mfumo wa 'quota system'.

Mfumo huo utawahitaji waagizaji wa ngano na shayiri nchini kununua kiasi cha shahiri na ngano kinachozalishwa ndani ya nchi kwa kila tani wanayoagiza kutoka nje ya nchi.

Hayo yalielezwa jana bungeni, na Wizara ya Kilimo katika majibu yake kwa Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Cecilia Pareso (pichani).




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

Katika kujenga swali lake, mbunge huyo alisema wakulima wa shayiri katika Wilaya ya Karatu wamekosa soko la uhakika la zao hilo kutokana na wanunuzi wakubwa ambao ni Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) kutonunua mazao hayo.

"Je, serikali inawasaidiaje wakulima hao?" mbunge huyo alihoji.

Katika majibu yake, wizara hiyo, ilisema lengo la mfumo huo ni kuongeza uzalishaji kwa wakulima wa ndani.

Wizara hiyo ilisema Kampuni za TBL na SBL huingia mikataba na wakulima kuzalisha shayiri kila mwaka.

Ilisema katika msimu wa 2018/19, TBL iliingia mkataba na wakulima kuzalishiwa tani 230 za shayiri kwa matumizi ya kiwanda.

"Kutokana na uzalishaji mkubwa wa wakulima, kampuni ilichukua shayiri kutoka kwa wakulima kwa awamu ambapo shehena ya mwisho ilichukuliwa kwa Sh. 800 kwa kilo," ilisema.

Hata hivyo, ilisema malalamiko ya soko la shayiri kwa wakulima wa Wilaya ya Karatu yametokana na wakulima kuzalisha shayiri nyingi nje ya mkataba wa kuzalisha ambapo kwa msimu wa 2018/19 ulikuwa tani 230.

"Kufuatia dosari hiyo, serikali iliwakutanisha kampuni ya TBL na wakulima ambapo ununuzi wa shayiri iliyozalishwa nje ya mkataba ulifanyika kwa bei ya chini ya ile ya mkataba, kampuni hiyo imelazimika kuihifadhi shayiri hiyo kwa muda mrefu kwa kuwa mahitaji ya kampuni ni tani 230 tu kwa mwaka," ilisema.



Wizara hiyo ilisema katika kuimarisha zao la shayiri nchini, serikali inaendelea na mpango wa kupunguza kodi kwa kimea kinachozalishwa na kusindikwa nchini. "Uamuzi huo unatarajia kuongeza uzalishaji wa shayiri na viwanda vinavyosindika shayiri nchini. Pia, serikali inaendelea kuwasiliana na TBL ambayo pia ni wamiliki wa kinu cha kusindika shayiri mkoani Kilimanjaro," ilisema.

Ilieleza kuwa pia inajipanga kufufua kinu hicho au kumpa mwekezaji atakayeweza kukiendesha ili kiweze kusindika kimea kinachozalishwa nchini.

Wizara hiyo ilisema hatua ya ufufuaji wa kinu hicho itawezesha kuongeza uzalishaji wa shayiri nchini na hivyo kuwanufaisha wakulima na kupunguza uagizaji wa shayiri kutoka nje ya nchi.

## Uboreshaji Sera ya Nyumba rasmi Juni

SERIKALI imesema ukusanyaji maoni ya wadau na uboreshaji wa Rasimu ya Sera ya Nyumba utakamilika ifikapo Juni mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi bungeni jana ilipojibu swali la Mbunge wa Babati Mjini (CCM), Pauline Gekul (pichani chini).

Mbunge huyo alihoji ni lini serikali itakamilisha Sera ya Nyumba na Makazi nchini.

Wizara hiyo ilisema serikali kwa kushirikiana na Mtaalamu Elekezi kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi, ilianza kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000 kwa lengo la kuihuisha ili iendane na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya sasa na miaka ijayo.

"Lengo la pili la kufanya mapitio hayo lilikuwa ni kutenganisha masuala ya nyumba na makazi ambayo yapo katika Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000 ili kuwa na Sera ya Taifa ya Nyumba inayojitegemea," ilisema.

Ilibainisha kuwa hadi sasa, Rasimu ya Sera ya Nyumba imeandaliwa kwa kushirikiana na Mtaalamu Elekezi na mpaka kufikia Februari mwaka huu, ukusanyaji wa maoni ya wadau ulikuwa umefanyika katika mikoa ya Mtwara, Ruvuma, Lindi, Mbeya, Songwe, Iringa, Rukwa, Mwanza, Kagera, Geita, Dodoma, Singida, Moshi, Manyara, Kilimanjaro na Tanga.

"Ni mategemeo yetu ukusanyaji maoni ya wadau na uboreshaji wa rasimu ya sera utakamilika ifikapo Juni, 2020, baada ya hatua ya kukusanya maoni kukamilika, maoni ya wadau yatajumuishwa katika Rasimu za Sera hiyo na hivyo kuendelea na hatua inayofuata ya uidhinishaji wa sera," ilisema.



Wanahabari walioandaliwa ni muhimu Uchaguzi Mkuu Ukurasa 13





Ukurasa 14

## Corona yawatia lawamani viongozi Ulaya, Marekani



Na Beatrice Moses

AJUAYE ni Mungu jinsi Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Assemblies of God Mikocheni B, Mlima wa Moto, Dk. Gertrude Rwakatare, alivyoingia kwenye siasa na kufanikiwa kuwa mbunge wa viti maalum, akiwa amebeba ujumbe wa Injili kila aliposimama.

Bungeni Dodoma kwenye vikao, karibu mara zote alipochangia hoja hakuionea haya Injili japo maneno machache, Bunge litakosa mahubiri huyu shujaa.

**KUPATA UBUNGE**

Ilikuwa mwaka 2005 alijitokeza kugombea ubunge kwa tiketi ya viti maalum, hata hivyo kura hakufanikiwa wakati huo hadi mwaka 2007 baada ya kifo cha aliyekuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Salome Joseph Mbatia.

Mbatia alikuwa ni Mbunge Viti Maalumu CCM aliyefariki kwa ajali ya gari Njombe mkoani Iringa, akiwa kwenye kampeni za kusaka ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa.

Dk. Rwakatare licha ya kuwa Askofu mbunge, pia alikuwa ni mmiliki wa Shule za St Mary's International na katika shughuli za uwekezaji alisifika kwa kiwango kikubwa ikiwamo kuwekeza kwenye maisha ya wahitaji na pia kina mama wengi.

Aidha, anatajwa kuwa mpenda watu na Februari mwaka huu, mbunge huyu wa viti maalum jimbo la Kilombero, alikabidhi pikipiki 22 kwa CCM ili zitumike kwenye kampeni za uchaguzi.

Awali alieleza kuwa alishakabidhi baskeli 300 kwa chama hicho ili kukisaidia kuleta maendeleo jimboni Kilombero.

Historia ya maisha ya kisiasa inaonyesha kuwa mwaka 2010 alishinda ubunge wa viti maalumu japo 2015 hakupata nafasi hiyo hadi 2017 alipoteuliwa kuziba nafasi ya Mwenyekiti wa UWT Sophia Simba, baada ya kuvuliwa uanachama CCM.

**MAOMBI MAALUMU**

Katika michango yake bungeni



Dk. Rwakatare muda mfupi baada ya kukabidhi pikipiki kwa Katibu Mkuu wa CCM , Dk. Bashiru Ali, (mwenye kofia ngumu) wilayani Kilombero mapema mwaka huu. **PICHA: BLOGI YA CCM**

# Buriani Dk. Rwakatare; Mchungaji, mbunge

> "Mheshimiwa Spika, naomba nyumba za askari Ifakara na Kilombero zijengwe, wana shida kubwa ya makazi.

ilidhihirisha nguvu ya kuhubiri ilivyokuwa ndani yake, wakati akichangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji, alianza:

"Awali ya yote ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema yeye ambaye ametupa zawadi ya uhai, ametupa zawadi ya afya, ametupa zawadi ya maji, ametupa zawadi ya ulinzi, na hakika tunasafiri na kurudi kwa sababu ya ulinzi wake. Mungu wetu ni mwema."

"....Ningependa kuchukua nafasi hii kumweka kila mmoja wetu hapa mikononi mwa Mungu aweze kuwatetea na kuwalinda kwenye majimbo yenu, kazi zenu ziweze kwenda salama."

" Lakini zaidi tuombe maombi rasmi kwa ajili ya Rais wetu John Magufuli, hakika kabisa tumepata chuma, tumepata jembe, lakini tumepata baba yeye....," alisema na kuongeza kuwa anaomba Rais apate kibali kwa Watanzania wote na jina lake liwe sukari midomoni, chumvi midomoni mwao na ulinzi wa Mungu uwe juu yake kwa jina la Yesu.

**DOKTA MENGI**

Dokta Rwakatare, alimkumbuka mfanyabiashara maarufu, Dk. Mengi, akisema

"Nachukua pia nafasi hii niweze kumkumbuka mheshimiwa Dk. Reginald Mengi, mfanyabiashara maarufu. Tukikumbuka katika bajeti ya maji, ndiye aliyeanzisha maji ya chupa Kilimanjaro, ameanzisha ITV, mambo mengi amefanya, ana huruma anakula na watu wenye shida, walemavu, kwa hivyo amefanya kazi nzuri Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi

Akichangia hotuba hiyo anasisitiza kuwapunguzia wanawake mzigo wa kusaka maji... "ningependa nijikite kwenye maji safi na salama mnajua maji ni kila kitu na lengo letu ni kumtua mwanamke ndoo ili aweze kupumzika maji yafike nyumbani.

Alibainisha kuwa anatokea Morogoro kwenye miito 177 ya kudumu na sio ile msimu, pia katika Wilaya ya Kilombero kuna mito 38 ya kudumu ya kudumu na ikujumlishwa ni mingi.

" Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba watu wengi hawajafikiwa na majisafi na salama inabidi wakachote mtoni, wakatafute ni shida. Lakini nilikuwa naomba katika bajeti hii Waziri utuhurumie watu wa Kilombero uweze kuangalia kwa maana maji yapo Mungu ametupa neema tatizo kubwa ni miundombinu

Tunaomba Waziri aiangalie Kilombero kwa huruma, tumevumilia miaka mingi. Nakumbuka ya kwamba miundombinu ile ilikuwa kama Ifakara mjini ilihudumia watu 7,000 enzi hizo sasa hivi watu ni takribani 300,000 mji wa Ifakara pekee. Kwa hivi tunaomba kwa kweli mtusaidie na sisi tupate majisafi na salama."

**POLISI IFAKARA**

Wakati akichangia mapato na makadirio ya fedha kwa mwaka 2019/2020 kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi -Rwakatare, licha ya kupongeza utendaji kazi wa polisi anaomba wajengewe nyumba.

"Mheshimiwa Spika, naomba nyumba za askari Ifakara na Kilombero zijengwe, wana shida kubwa ya makazi,"

Pia aliomba Mahakama ya Ifakara ijengwe kwa kuwa, wakati wa masika mafuriko yanaathiri wafungwa, mafaili, ofisi, hivyo ni kero kubwa..

Dk Rwakatare alipenda elimu na alikaririwa akichangia pia kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

## Dk. Bashiru: Kugawa sukari na vitenge ni matusi kwa mpigakura Ukurasa 12

# Dk. Bashiru: Kugawa sukari na vitenge matusi kwa mpigakura

**Na Sabato Kasika**

TANZANIA inatarajia kufanya uchaguzi mkuu mwishoni mwa mwaka huu na tayari baadhi ya wanasiasa wameshatangaza kustaafu siasa, huku wengine wanajipanga kujitosa kuwania jukumu la kuwawakilisha wananchi wao.

Wakati joto la uchaguzi huo likiendelea kupanda, makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamekumbushwa kuzingatia ahadi za mwanachama, ili kuepuka mtego wa kuingia katika rushwa.

CCM inawakumbusha wanachama wake kuzingatia hilo kwa vile lipo kwenye ahadi 10 za mwanachama, ambazo zinaelezwa kuwa zikizingatiwa na kila mwanachama zitakuwa ni mwiba wa rushwa.

Hilo linahimizwa, kwa vile linasaidia kufanya mchakato wa kupata wawakilishi wa chama kwenye uchaguzi mkuu kuwa wa haki na kuendelea kukijingea chama heshima mbele ya jamii.

Maelekezo hayo ni ya Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, ambaye anawataka wanachama kusimamia misingi ya haki katika mchakato wa kuwapata makada wa kuwakilisha chama katika uchaguzi mkuu.

Katika moja ya vikao vyake na viongozi wa chama hivi karibuni, katibu huyo anasema, ahadi za uanachama ndizo msalaba wa mwanachama, hivyo kila mmoja hana budi kuzingatia.

Katibu Mkuu Bashiru anasema, amepata habari, zikiwamo za ukweli kwamba, makada wanaotaka kutia nia, baadhi yao wanataka kuendelea na wengine wanawania, wanafanya dharau kwa wapigakura.

"Wanazunguka na sukari na vitenge na Sh. 5,000 na 10,000, hiyo ni dharau na matusi kwa wapigakura waache. Wewe kama una sifa, kwa nini unahangaika kujipaka wanja, hatutafuti mrembo tunatafuta kiongozi bora," anasema Dk. Bashiru.

Anasema, wapo makada wanaozunguka na wajumbe na kwamba viongozi hao wenyewe wanajidhalilisha bila kujua kuwa siku hizi kuna teknolojia inayofuatilia nyendo zao ikichukua sura na sauti.

"Mtu mzima anazungushwa na mtu mzima mwenziye, tusiache misingi ya kusimamia uchaguzi wa haki kwenye uteuzi, na ndugu zangu kura za maoni ni mapendekezo, vikao ndivyo vinateua," anasema.


Katibu huyo anawataka wajumbe wa vikao vya uteuzi wasikubali kununulika, kwa vile rushwa ni adui wa haki, anataja rushwa hiyo ya Sh. 5,000 na 20,000 kuwa ni ya dharau.

"Thamani ya uongozi uliopewa na chama chako ni kubwa, chama cha Mwalimu Nyerere, aliyekufa bila kupokea rushwa, na wewe umeapa kwamba rushwa ni adui wa haki hutatoa wala kupokea. Halafu kwa kificho unasogezewa hela kwenye simu yako, eti uje umfikirie Bashiru anataka kugombea anatangaza nia, hata kama hatukuoni, nafsi yako ikusute, tuongozwe na busara zaidi," anasema.



Dk. Bashiru akizungumzia masuala mbalimbali ya CCM. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> Makatibu wa CCM kila ngazi hata nyie msiwe wa kupokea rushwa kupitisha majina ya wagombea wasiokuwa na sifa lazima kiongozi afuate miiko na ahadi za mwanachama.



Vitenge moja ya 'mlungula' unaotolewa na watiania pamoja na wagombea kununua wapigakura.

Kiongozi huyo anawataka wanachama wasikifanye chama hicho kuwa cha kipolisi, kwamba nani yuko wapi, Dk. Bashiru yuko wapi, bali ahadi za mwanachama ziwe ndiyo msalaba wao.

## AHADI KUMI

Katika ahadi hizo za mwanachama, ya kwanza inasema binadamu wote ni ndugu zangu na Afrika ni moja, wakati ya pili inasema nyingine ni kujibebesha jukumu la kuitumikia nchi kuwa nitaitumikia nchi yangu na watu wake wote.

Ahadi ya tatu ni kujitolea ikisema nitajitolea nafsi yangu kuondoa umaskini, ujinga, magonjwa na dhuluma, huku ahadi ya nne ikisema rushwa ni adui wa haki. Sitapokea wala kutoa rushwa.

Ya tano inahusu uongozi kuwa cheo ni dhamana. Sitakitumia cheo changu wala cha mtu mwingine kwa faida yangu, ya sita inajikita kwenye elimu kuwa nitajielimisha kwa kadiri ya uwezo wangu na kutumia elimu yangu kwa faida ya wote.

Kwa upande wa ahadi ya saba, inahimiza kushirikiana, mwanachama akisema nitashirikiana na wenzangu wote kuijenga nchi yetu, wakati ya nane inawataka kuwa wakweli, kwa kusisitiza kuwa nitasema kweli daima, fitina kwangu mwiko.

Uaminifu ni ahadi ya tisa inayosema, nitakuwa mwanachama mwaminifu wa CCM na raia mwema wa Tanzania na Afrika, huku ya 10 ikitaka kutii, nitakuwa mtiifu na mwaminifu kwa Rais wa Serikali ya Tanzania.

## UKIUKAJI AHADI YA 8

Kinachosisitizwa na Katibu Mkuu Bashiru kwenye ahadi ya nne, ambayo inakemea rushwa kwa vile inasababisha baadhi ya watu kukosa haki, hivyo ni muhimu mchakato wa kupata viongozi ipitie njia sahihi.

Katibu huyo anasema, kada atakayejihusisha na vitendo vya rushwa katika mchakato wa chama hicho wa kusaka wagombea wake katika uchaguzi mkuu, atapoteza sifa za kugombea.

Kwamba kila atakayejitokeza kugombea uongozi, lazima awe mwadilifu na mwaminifu, na kuongeza kuwa baadhi ya wagombea wanatumia majukwaa kupinga rushwa licha ya kuwa wanajihusisha nayo.

"Makatibu wa CCM kila ngazi hata nyie msiwe wa kupokea rushwa kupitisha majina ya wagombea wasiokuwa na sifa lazima kiongozi afuate miiko na ahadi za mwanachama," anasisitiza.

Anasema, rushwa ni sawa na usaliti ndani ya chama, kwamba wanachama wanauza kura, hakuna wanachokipata zaidi ya kujidhalilisha na kuuza utu wao kwa watu wasiokuwa na sifa za uongozi.

"Vita dhidi ya rushwa ni suala la imani ambayo kila mwanachama anapaswa kuitekeleza. CCM mpya chini ya mwenyekiti wake Rais Dk. John Magufuli haitamvumilia wala kumwonea kiongozi au mwanachama yeyote atakayejihusisha na rushwa," anasema Dk. Bashiru.

UCHAMBUZI

# Wanahabari walioandaliwa ni muhimu Uchaguzi Mkuu

Na Mwandishi Wetu

MOJA ya changamoto zinazoweza kuibuka na kusababisha kuyumba kisiasa kwa taifa ni mchakato wa uchaguzi mkuu ambao mara nyingi kama hauna uwazi, haki na uhuru huishia kulalamikiwa na wakati mwingine husababisha machafuko kutoka kwa wale ambao wanadhani hawakutendewa haki.

Lakini, hawa wanaolalamika wanategemea kujenga hoja zao ama kupitia au kutoka kwenye taarifa za vyombo vya habari ambavyo huhusika moja kwa moja kutoa habari za mchakato wote kuanzia usajili wa wapigakura, kampeni, siku ya uchaguzi, kutangaza matokeo, kuapishwa na mambo mengine yanayofuata.

Kwa hiyo wanahabari ni wadau wakuu wa mchakato huu, wanapaswa kuandaliwa ili kusaidia kuelimisha jamii kuepusha changamoto zinazoweza kuleta maafa baada ya uchaguzi mkuu, ndiyo maana mwaka huu ambao kuna uchaguzi mkuu licha ya kuwapo corona, wapigakura pamoja na wanahabari wanatakiwa kuzingatia umuhimu wa kuripoti taarifa zinazolenga kupunguza madhara na kuongeza ufanisi kwenye uchaguzi ili kuendelea kuleta amani na maendeleo.

Hayo ni baadhi ya mambo muhimu yanayohitajika kupewa kipaumbele ili kufanikisha kuandika habari za uchaguzi kwa maslahi ya taifa.

Ni ukweli kuwa waandishi ni daraja linaunganisha wapigakura na wadau wengine kuanzia, vyama vya siasa, waangalizi wa uchaguzi, wasimamizi, serikali na wagombea, hivyo huhitaji kuandaliwa kikamilifu na pia kujipanga ili kuepusha shari.

Wanahabari na wanasiasa wajue kuwa jukumu lao kubwa ni kutoa taarifa za kulinda amani, zinazohimiza wanachama na wadau kudhibiti matarajio yao ili kukubaliana na hali iwapo watashinda ama kushindwa uchaguzi.

Lakini, pia si waandishi peke yao aidha, vyama vya siasa vishirikiane na tasnia ya habari kuweka kwenye mizania masuala ya usawa wa kijinsia, kueleza jinsia wanavyowashirikisha wanyonge-walemavu, wanawake kwani mara nyingi habari za wanawake na makundi ya wanyonge mara nyingi husahaulika.

Ni wazi kuwa jukumu la kuwafikishia wananchi wa kawaida habari wakiwa mijini na vijijini na walioko pembezoni ni jambo jema lakini pia ni muhimu kuwawezesha wananchi hao nao sauti zao zisikike na wenyewe wawe sehemu ya wazungumzaji na watoa taarifa zinazohusu maisha yao kwenye uchaguzi mkuu.

Katika mwaka huu wa uchaguzi wadau wakiwamo vyama vya siasa wanatakiwa kushirikiana na wanahabari kuboresa uandishi na kuongeza uwajibikaji unaoleta mabadiliko na maendeleo kwa jamii



Wanahabari ni daraja muhimu kwenye kutangaza habari za uchaguzi zinazowanufaisha wapigakura, wagombea na wadau wengine. Elimu kwa mpigakura na waandishi pia kuheshimu tasnia ya habari vitasaidia kufikia azma hiyo. **PICHA: MTANDAO**

> Hayo ni baadhi ya mambo muhimu yanayohitajika kupewa kipaumbele ili kufanikisha kuandika habari za uchaguzi kwa maslahi ya taifa.

zote. Uandishi wa kuboresha na kuleta ufumbuzi badala ya kulalamika zaidi, kutukanana na kukosoana kusikokuwa na tija pamoja kutoa kauli za kujisifu na kutishia wengine usipewe nafasi.

Uandishi wa habari unafanikiwa iwapo wadau wa uchaguzi, wagombea, wasimamizi na mashirika ya kiraia (CSOs) watachangia kuhamasisha na kutoa habari za kudumisha amani, kuhimiza kuwapo uwazi na uwajibikaji katika uandishi na utoaji wa taarifa za kuaminika zinazohusu mchakato wa uchaguzi.

Uandishi wa kujihami ni muhimu kwa kuzingatia kuwa wakati wa uchaguzi kuna mihemko na matarajio makubwa hasa kwa watu wanaotegemea kuwa watashinda na wapo wanachama wasiotegemea kushindwa. Ni vyema wanachama na wapiga kura wakaelezwa kuwa penye ushindani kuna mmoja anaibuka mshindi.

Hapo ndipo kunapokuwa na umuhimu wa kufanyakazi na wanahabari wawe redio na televisheni za kijamii (community radio, TV) , blogi, redio na magazeti ya mitandaoni na ya kitaifa kwa pamoja kuhakikisha kuwa uchaguzi hauwi chanzo cha kuvunjika amani kwa wale watakaoona hawajashinda na kuhisi kuwa hawakutendewa haki.

Wakati mwingine kuvunjika amani kunaweza kusababishwa na kukosekana kwa taarifa sahihi mathalani, linapozungumziwa suala la umbali wa kusimama baada ya kupiga kura, lakini pia ni jukumu la wanahabari na wadau kutafuta ufafanuzi na ukweli kutoka vyanzo halisi hivyo iwapo wana habari wakijifunza kikamilifu watatimiza wajibu kwa kutoa taarifa za ufasaha na za kueleweka zinazosaidia umma kuelewa na kuondoa taarifa zinazoongeza sintofahamu au kusababisha watu kuwa na fikra na mihemko inayoweza kuvuruga amani.

### KUTOA UFAFANUZI

Katika matukio yanayosababisha sintofahamu vyombo vya habari ni daraja la kutoa maelezo na ufafanuzi wa masuala yanayoleta maswali mengi kuliko majibu na kuongeza hofu ama chuki miongoni mwa wananchi dhidi ya mamlaka za kusimamia uchaguzi.

Mathalani, wakati huu kumekuwa na madai ya kupata Tume Huru ya Uchaguzi kufuatia takwa hilo, wana habari wanatakiwa kupunguza mgawanyiko huo kwenye kuandika na kuonyesha kuwa hata bila kuwa na katiba mpya au tume hiyo, uchaguzi unaweza kufanya na ukawa wa huru na haki kwa kuzingatia ukweli na uwazi.

Kuendelea kuandika au kuripoti taarifa za upande mmoja bila ufafanuzi kunaweza kungeza mvutano kati ya CCM na upinzani. Hata hivyo, si vibaya kuendeleza masuala ya wanasiasa kuungana na kuwa na nguvu zaidi ikiwa ni pamoja na kuweka mgombea mmoja hivyo kuongeza hamasa na kuleta ushindani zaidi katika uchaguzi.

Kuendelea kuhamasisha taarifa za umoja na ushirikiano miongoni mwa wanachama kunapunguza mukari hivyo kudhibiti matarajio makubwa waliyo nayo baadhi ya wanachama na wapiga kura kwenye matokeo ya uchaguzi kwa vile katika kushindana kuna kushindwa pia, hivyo wale watakaoshindwa kukubali kufuata taratibu na kuendelea na amani na utulivu kwa manufaa ya taifa.

### USAWA KIJINSIA

Mara nyingi katika kampeni za uchaguzi masuala ya kijinsia hasa ya wanawake, vijana na wenye ulemavu yanasahaulika, hivyo wanahabari hawana budi kukumbusha na kuweka ajenda hiyo mbele ili ipate nafasi na pia kulenga mambo yanayohusu au yanayoathiri watu kwa mfano utekelezaji wa ahadi za wagombea. Kufuatilia na kuona iwapo serikali inashughulikia mambo yenye taathira kwa wanawake mfano mimba za utotoni, ukeketaji, sheria zinazokandamiza wanawake na watoto, mfano ndoa ambayo imeelekezwa na mahakama ifanyiwe marekebisho, kukosa elimu miongoni mwa mabinti na migogoro ya ardhi vijijini inayosababisha wanawake kukosa na kushindwa kumiliki ardhi.

# Corona yawatia lawamani viongozi Ulaya, Marekani

• Waulizwa ilizukaje, serikali zililala wapi?



Athari za ugonjwa wa corona nchini Marekani na mataifa ya Ulaya umewaweka kwenye hatihati viongozi wakuu wa nchi hizo, raia wakihoji ilikuwaje kupuuza maradhi bila kuchukua tahadhari hadi ugonjwa ukafikia hatua ya kuua maelfu? . **PICHA: MTANDAO.**

**Na Michael Eneza**

UTHABITI wa uongozi ulioko madarakani katika nchi kadhaa kubwa kiuchumi umeingia mashakani baada ya kutokea nyufa katika ngazi za juu za serikali na vyombo vya dola, nini ambacho serikali zilifanya hata corona ikalipuka katika nchi hizo. Hali hiyo imezikumba Uingereza na Italia, wakati hivi karibuni Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson alitoka chumba cha uangalizi wa karibu hospitalini St Thomas, halafu anasukumiwa lawama za uzembe na kuachia corona ipae. Nchini Italia mzozo haukuwa mkubwa, licha ya kuwa ni nchi yenye uzoefu wa mizozo kisiasa.

Nchini Uingereza zogo lilitokana na baadhi ya wakuu wa idara za serikali ikiwamo Cobra, kifupi cha 'Consolidated Budget Reconciliation Act,' sheria inayounda kitengo muhimu cha kutafuta fedha kutatua masuala ya dharura kitaifa au kikanda, barani Ulaya. Wataalamu wenye nafasi katika shughuli za kitengo hicho walivujisha taarifa katika gazeti moja maarufu la kila

> "Moja baada ya nyingine ngome hizo zilianza kuanguka, na ilipofikia hapo wataalamu wanaanza kutoa lawama hawakusikilizwa na wanasiasa!

Jumapili, 'Sunday Times' kuwa Waziri Mkuu 'alikacha' vikao vitano vya kujadili wimbi la corona lililokuwa linakaribia, kwa siku 32. Inaelekea ni kuanzia Februari hadi mwezi uliopita.

Mawaziri tofauti ambao nyadhifa zao zinaguswa na wimbi la corona walijitahidi kueleza nini hasa kilitokea, na kinachoonekana ni kuwa ni mikutano ya kitaaluma na kupanga sera kuhusu suala hilo, ambayo haikuwa inahitaji Waziri Mkuu binafsi awepo . Baadhi ya wachambuzi wa habari walielewa kisa cha ugomvi huo kuwa ni jambo la kawaida kwa watalaamu kutaka awepo mkuu wa nchi (huku kwetu au mkuu wa serikali ng'ambo, na Marekani angekuwa ni Rais Trump mwenyewe) ambaye wangetaka awepo. Wanatazamia akiwapo atapitisha, si angoje maelekezo.

Nchini Marekani, ugomvi kuhusu kulipuka kwa corona kulianza katika kuushambulia utawala wa Donald Trump kuwa ulipuuzia suala hilo, na baadhi ya watu wake wa karibu wakihojiwa kwa mfano na televisheni ya Fox Channel inayopendwa na wahafidhina nchini humo, walikataa kabisa kuwa ipo hatari. Ni kielelezo cha viashiria vya kibaguzi vilivyoanza kujitokeza tangu mwanzo wa wimbi la corona, watu wakijaribu kujitofautisha na kutoa sababu fikirika za kiitikadi kwanini nchi hiyo au watu hao hawatasumbuliwa na corona. Moja baada ya nyingine ngome hizo zilianza kuanguka, na ilipofikia hapo wataalamu wanaanza kutoa lawama hawakusikilizwa na wanasiasa!

Ni kweli kuna wakati Rais Trump alizungumzia 'the Chinese virus,' kirusi cha Kichina, kwa kejeli fulani. Suala hilo lilipolipuka Marekani akaona alibebeshe lawama Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa ushauri mbaya, akakata fedha Marekani inazotoa huko. Ni asilimia 15 ya bajeti ya shirika hilo, akisema walitoa ushauri mbaya hasa kusisitiza kuwa China isitengwe, wasizuie safari za ndege, kuwa kufanya hivyo ni ubaguzi, hivyo Marekani ikakanywa isijizatiti.

Upande wa pili wa shilingi ni ushindani wa kiitikadi kuhusu hatua za kisera kupambana na wimbi la corona, ulioendeshwa hasa kati ya Rais Trump na Gavana Andrew Cuomo wa jimbo la New York, ambalo kwa kipindi kirefu lilikuwa na nusu ya idadi ya maambukizi yote nchini humo. Kwanza kulikuwa na suala la kuzuia usafiri kati ya New York na miji mingine mikubwa Marekani, alilotaja Trump awali, gavana akasema haelewi hisia hiyo inalenga nini, na kwa hali yoyote ile haitekelezeki. Ikababakia tu watu kuzuiwa au kuhimizwa wabaki nyumbani, wasitoke.

Kinachoendelea katika nchi nyingi ukanda wa kaskazini ni kuanza kufungua milango na kurejesha shughuli za kawaida kwa hatua, licha ya kuwa zinatofautiana nini kifanyike. Yako maeneo ambako hatua zinachukuliwa kitaifa hasa Ulaya, lakini Marekani masuala ya usimamizi wa mapambano dhidi ya corona ni ya jimbo, serikali ya shirikisho ikiwa inatoa miongozo ya jumla pale inapohitajiwa (kwa mfano kuzuia safari za anga kwenda Ulaya au kuingia Marekani kutoka Ulaya). Ni moja ya maeneo yaliyopigiwa kelele sana, wakati nchi za Ulaya ni maswahiba wa Marekani hivyo kuweka vizuizi hakukuonekana kama ni ubaguzi.

Moja ya sauti zilizosikika kwa nguvu kuhusu suala hilo nchini Marekani hivi karibuni ni ile ya rais mstaafu Barack Obama, ambaye sasa anajisikia huru zaidi kuchangia au kutoa hoja katika masuala muhimu ya nchi. Ni baada ya makamu wake akiwa madarakani, Joe Biden kukaribia kabisa kutangazwa mshindi wa kinyang'anyiro cha mgombea urais wa chama cha Democratic katika uchaguzi mkuu Novemba mwaka huu. Anasisitia kuwapo upimaji kwa kiwango kikubwa ili walioambukizwa wagunduliwe mapema na walio na afya nzuri wasizuiliwe kujitafutia riziki.

Kabla ya suala la kueneza vifaa vya upimaji (kwa mfano kipima joto mwilini kuona kama kuna dalili za mbali za corona) kupewa kipaumbele, Rais Trump alishatoa rai kuwa vizuizi viendelee kuwekwa hasa kwa wazee wa zaidi ya miaka 60.

Alisema vijana hasa wale wenye umri usiozidi miaka 40 wasizuiliwe kwani hata wakipata virusi vya corona haviwasumbui zaidi ya kupata tembe kadhaa na kupona haraka, tofauti na watu wenye umri mkubwa na hasa wenye magonjwa ya ziada. Licha ya kuwa alipingwa sana kwa hoja kuwa 'hawasikilizi wataalamu,' ambao wakati huo walikuwa wanalenga zaidi hatua kuzuia ueneaji wa maambukizi, sasa hilo halina ubishi tena.

Kilichowarudishia watu matumaini ni kutaka vizuizi viondolewe ni mpangilio wa kupata corona na kupona au kufa, kuwa walio hatarini hasa ni wenye magonjwa ya moyo, presha, kisukari na udhaifu mwingine, si kila mtu. Ikafikia mahali Rais Trump, akiwa analenga kuwakusanya wafuasi wake kwa ajili ya uchaguzi mkuu baadaye, akawashambulia magavana wa Democratic wanaong'ang'ania vizuizi, hata kuchochea maandamano. Aliishangaza dunia kwa kuandika katika ukurasa wa twitter kuwa kuna haja kukomboa 'liberate' baadhi ya majimbo.



# Vijana wataka kuongezewa muda kurudisha mikopo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

VIJANA walio kwenye vikundi vya kunufaika wa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma, wameomba serikali kuwaongezea muda wa kufanya marejesho kutokana na miradi yao kuathiriwa na mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa kikundi cha Tusumuke Group, kinachojihusisha na uzalishaji kuku, ufugaji kuku pamoja na utoaji wa elimu ya ufugaji, Christopher Dioniz, wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Dioniz alisema kutokana na uwapo wa corona, mradi wao umeathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na kushindwa kusambaza kuku katika maeneo ambayo walikuwa wanapeleka awali kabla ya mlipuko huo wa virusi vya Covid 19.

Alisema kikundi chao hivi sasa kinauwezo wa kuzalisha vifaranga 31,000 kila mwezi, lakini hakuna soko kutokana na mlipuko wa virusi vya ugonjwa wa corona ambao unazidi kusambaa katika maeneo mengi ya nchi.

"Kabla ya ugonjwa huu kuingia tulikuwa na uwezo wa kuuza kuku 50 hadi 100 kwa siku, lakini baada ya corona kuingia tumeshuka sana kibiashara, tunauza kuku 10 hadi 20 kwa siku hivi sasa," alisema Dioniz.

Vile vile, alisema soko lao limeshuka kutokana na kutegemea wateja wa hoteli, nyumba na mikoa ya jirani, lakini hivi sasa wamesitisha usafirishaji wa kuku pamoja na vifaranga hadi hapo hali itakapo kuwa shwari.

Pia, alisema katika miaka ya nyuma kipindi cha Sikukuu ya Pasaka walikuwa wanauza kuku 500, lakini mwaka huu kutokana na corona wameuza kuku 150 pekee.

Aliomba serikali baada ya mlipuko wa ugonjwa huo kupita ifanye tathmini ya hasara zilizotokea katika vikundi ambavyo vilipatiwa mikopo ya asilimia 10 na halmashauri zao ili kuvisaidia kuongeza muda wa kufanya marejesho.



Askofu mstaafu wa kanisa la PHAM (T), Mtera Staaf Mwandambo (aliyeshika kipaza sauti), akiiombea bendera ya taifa kama ishara ya alama ya nchi ya Tanzania kwenye maombi yaliyofanyika kijiji cha Mtera kilichopo wilayani Mpwapwa jana ili Mungu aepushe gonjwa la korona ambalo limekuwa tishio nchi mbalimbali hapa duniani.**PICHA: PETER MKWAVILA**

## Waomba vipima joto kwenye mikusanyiko

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Maridhiano mkoani hapa, Evance Chande, ameiomba serikali kuweka utaratibu wa kuwapo vipima joto kwenye maeneo ya mikusanyiko ya watu.

Chande alisema licha ya mkoa kuchukua hatua mbalimbali ya kuweka vifaa vya kujikinga na maambukizi hayo ya corona pia ni muhimu ikawapo huduma ya upimaji kwa kila mtu kwenye maeneo ya mikusanyiko.

Kiongozi huyo pia aliomba barabara zote zinazoingia kutoka mikoani na wilayani kuweka vizuizi ambavyo vitakuwapo pia na vipimo hivyo.

Ushauri huo ulitolewa na mwenyekiti huyo wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema kuna umuhimu mkubwa kwa mkoa huo kuwapo kwa tahadhari hiyo ya kipima joto ikizingatiwa kuwa ni makao makuu na mwingiliano mkubwa wa watu kutoka maeneo mengine.

"Mfano mzuri ambao tayari umeshaanza ni pamoja ofisi za bungeni na hospitali ya Benjamini Mkapa ambako watu wanaoenda kwenye maeneo hayo hulazimika kupima kila mtu," alisema.

Hata hivyo, amezipongeza taasisi na mashirika mbalimbali zikiwamo za kidini na wanasiasa kwa kuiunga mkono serikali katika jitihada za kutoa vifaa na elimu juu ya ugonjwa huo.

Alisema juhudi hizo zinazofanywa zinasaidia watu kutambua athari za ugongwa ambao umetikisa karibu ulimwengu wote.

# Maofisa wahimizwa kutoa elimu vijijini

**Na Peter Mkwavila,** MPWAPWA

UMOJA wa Makanisa ya Kipentecost Mtera wilayani Mpwapwa, umewataka viongozi wa siasa kutobweteka ofisini kwa kuwa bado kuna kundi kubwa linahitaji kuelimishwa ugonjwa wa corona.

Katika hatua nyingine, umoja huo wa madhehebu ya dini pia umewaomba viongozi wa dini kwenda kwa waumini wao wanaoishi vijijini kwa ajili ya kuwapatia elimu ya jinsi ya kujihadhari na ugonjwa huo.

Askofu wa Kanisa la Evangelistic Assemblies of God Tanzania (EAGT), Jackson Madelemu, alisema hayo kwa niaba ya umoja huo kwenye hitimisho la maombi ya siku tatu ikiwa ni sehemu ya kuitikia wito wa Rais Dk. John Magufuli. Alisema kuwa wakati huu siyo wa kukaa ofisini na kanisani wakiwa mijini na kusubiri taarifa, bado kuna makundi yanahitaji kuelimishwa janga hilo la corona.

Akizungumza kwenye maombi hayo yaliyofanyika viwanja vya Kanisa la Bonde la Baraka EAGT Mtera, alisema kuwa vijijini bado hawana uelewa wa janga hilo tofauti na mijini ambako elimu imefanikiwa kwa sehemu kubwa.

Kwa upande wake Askofu mstaafu wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission (T), Asswille Mwandambo, aliwataka Watanzania kufuata maelekezo yanayotolewa na viongozi na wataalamu wa afya ili taifa liepuke balaa hilo.

Aliwataka pia Watanzania kufanya kazi kwa bidii kwenye maeneo yao badala ya kutanguliza hofu na kushindwa kujiingizia kipato.

"Pamoja na janga hili kuwa kubwa, tusiache kumuomba Mungu na kufanya kazi zitakazo tuingizia kipato ambacho kitainua uchumi wetu hapa nchini," alisema.

Naye Katibu wa Umoja huo wa madhehebu ya Mtera, Mchungaji Franco Ndenda, alisema maombi hayo yamefanyika kwa malengo ya kuitikia agizo la Rais Magufuli ambaye aliwataka Watanzania kumuomba Mungu ili aondoe balaa hilo la corona.

Ndenda ambaye ni Kiongozi wa Kanisa la Full Gospel Bible Fellowship, pia aliwataka Watanzania kutoudharau ugonjwa huo badala yake waheshimu mamlaka husika.



## Wakulima waingia hofu kushuka zao la kahawa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wakulima wa kahawa mkoani Mbeya, wameanza kupata wasiwasi wa kushuka kwa soko la zao hilo kutokana na tishio la ugonjwa wa Corona wakidai kuwa wanunuzi wengi wa zao hilo ni kutoka nje ya nchi.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti juzi, wakulima hao katika bonde la Utengule katika Mamlaka ya mji Mdogo wa Mbalizi, walisema wanapata hofu hiyo kutokana na mipaka ya mataifa mengi kufungwa.

Mmoja wa wakulima hao, Joseph Mwashitete, alisema kahawa ni tofauti na mazao ya chakula na soko lake la ndani ni dogo kuliko la nje na wanazalisha zao hilo kutokana na hamasa wanayoipata kutokana na soko la nje.

Alisema baadhi ya kampuni kutoka nje ya nchi zimekuwa zikiwakopesha pembejeo kwa ajili ya zao hilo, lakini kwa sasa kuna hatari ya mikopo hiyo kusitishwa na uzalishaji kuporomoka.

"Mazao ya chakula hata tusipouza huwa tunakula wenyewe, lakini kahawa hata gunia moja mimi na familia yangu hatuwezi kutumia tukamaliza kwa mwaka, sasa mataifa tunayoyategemea ndiyo yanayokabiliwa kwa kiasi kikubwa na tatizo la corona," alisema Mwashitete.

Alisema wasiwasi mkubwa wanaupata kutokana na serikali za mataifa mengi kuanza kusitisha mwingiliano wa watu ikiwamo kusitisha safari za ndege za abiria.

Naye Nathan Mbwaga, mkulima wa kahawa katika Kijiji cha Itimba, alisema msimu wa kahawa kuanza kuchumwa unakaribia, lakini mpaka sasa kampuni zilizoanza kuonyesha nia ya kwenda kununua ni chache.

Aliiomba serikali kuendelea kutoa elimu kwa wananchi wa kada zote ili ugonjwa huo usiendelee kuenea kwa kuwa ukisambaa hata soko la ndani la kahawa litakuwa dogo.

Alisema uzalishaji wa zao hilo umekuwa ukiongezeka kila mwaka kutokana na mahitaji ya soko la dunia na kwamba kwa sasa wana wasiwasi kuwa hata kiwango cha uzalishaji kitashuka kutokana na kuporomoka kwa soko.

# Chalamila asitisha uhamishwaji wafanyabiashara

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MKUU Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amesitisha mpango wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe wa kutaka kuwahamisha wafanyabiashara wa ndizi wanaofanya shughuli zao kando ya barabara katika eneo la Kiwira wilayani humo kwenda mahali pengine walipowaandalia.

Chalamila alifikia uamuzi huo juzi baada ya kubaini kuwa eneo ambalo limeandaliwa na halmashauri hiyo ni dogo na halina miundombinu inayoweza kukidhi mahitaji ya wafanyabiashara hao.Kabla ya kutoa uamuzi huo, Chalamila aliwatembelea wafanyabiashara hao kwenye eneo lao la Kiwira kuwapatia elimu kuhusu ugonjwa wa corona nao kumweleza kero yao.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyabiashara wenzake, Janeth Mwalwiba, alisema eneo walilotengewa wakafanyie kazi zao ni dogo na haliwezi kuhimili wafanyabiashara wote wa ndizi waliopo mahali hapo.

"Hapa tupo wafanyabiashara zaidi ya elfu moja, eneo lililoandaliwa kwa ajili yetu halitoshi maana tukienda tutaweza kupanga meza zetu tu na sisi tutakosa hata mahali pa kusimama, hivyo tunaomba tuendelee kubaki hapa maana ndipo panapokidhi mahitaji yetu," alisema Janeth.

Akizungumzia malalamiko ya wafanyabiashara hao, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, alisema katika vikao vyao walikubaliana kuwahamisha wafanyabiashara hao kutoka kwenye eneo hilo baada ya halmashauri kuwaandalia eneo lingine na kuwawekea miundombinu na mazingira ya kufanya biashara.

Alisema katika eneo hilo walioandaliwa ilitakiwa liwe na kituo cha mabasi ya abiria ambayo yatasimama kushusha na kupakia abiria ili wafanyabiashara hao wapate wateja kama ilivyo katika eneo walilopo hivi sasa.

Chalya alisema kuwa hivi karibuni aliarifiwa na halmashauri kuwa imekamilisha maandalizi ya eneo hilo na kwamba wafanyabiashara hao wanaweza kuhamishiwa huko kwa vile eneo hilo lipo tayari.

Alisema baada ya kupata taarifa hiyo ofisi yake ililitembelea na kubaini kuwa eneo lililoandaliwa ni dogo na pia miundombinu hasa barabara za magari ya abiria za kuingia na kutoka sio mizuri.

"Tulipolitembelea eneo hilo tukabaini kuwa halijakamilika, kwanza ni dogo na miundombinu yake sio mizuri, tunaamini wafanyabiashara hawa wakihamia pale kwa sasa kunaweza kutokea ajali za mara kwa mara na kuhatarisha maisha yao," alisema Chalya.

Pia, alisema ameiagiza halmashauri kuendelea na matengenezo ya eneo hilo na kulikamilisha kabla ya kuwahamisha wafanyabiashara hao.

Baada ya kupata maelezo hayo, Mkuu wa Mkoa, Chalamila akatangaza kusitisha mpango huo na kuwataka wafanyabiashara waendelee na kazi zao mpaka hapo watakapopata maelekezo mengine kutoka kwake.

"Katika kipindi hiki ambacho taifa linapambana na corona, sio vizuri kuendelea kusumbuana, naagiza sitisheni kwanza mpango wa kuwahamisha wafanyabiashara hawa, waacheni waendelee na kazi zao wakiwa hapa hapa mpaka nitakapotoa maelekezo mengine," alisema Chalamila.

Alisema bidhaa za wajasiriamali hao ambazo ni matunda ya maparachichi, ndizi na mananasi ambayo hayapaswi kukaa muda mrefu bila kutumika kwa vile yanaharibika haraka.

"Ninyi wafanyabiashara tafuteni wateja popote mnapoona mnaweza kuwapata ili mradi muuze bidhaa zenu, kama ni makanisani uzeni, misikitini uzeni, sokoni uzeni na hata hapa barabarani nyie fanyeni kazi," alisema Chalamila. Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Ezekiel Mwankota, alisema amepokea maelekeo ya Mkuu wa Mkoa na kuahidi kuwa yatafanyiwa kazi na halmashauri yake.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kushoto), akizungumza na baadhi ya wajasiriamali wanaouza matunda katika eneo la Forest ya zamani jijini Mbeya, aliwataka wazingatie maelekezo ya wataalamu wa afya ikiwamo kunawa mikono ili kuepuka maambukizi ya virusi vya Corona. **PICHA NA NEBART MSOKWA.**

# Wastaafu watarajiwa watahadharishwa dhidi matapeli

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

WAFANYAKAZI mkoani hapa, wametakiwa kuwa makini na genge la watu wanaopita katika ofisi za halmashauri mkoani humo na kuwahadaa kwa kujitambulisha kuwa wanatoka katika Ofisi ya Rais Utumishi na Tamisemi, wakidai kutaka kuwasaidia wafanyakazi wanaotarajiwa kustaafu na kuhama vituo vyao vya kazi kutokana na taarifa zao kutokuwa sahihi.

Kwa mujibu wa taarifa ndani ya halmashauri tofauti mkoani hapa genge hilo la matapeli limekuwa likiwahadaa wafanyakazi hao na kujipatia fedha wakidai kuwasaidia wafanyakazi wanaotarajia kustaafu na waliokwama kutokana na changamoto za taarifa zao za kiutumishi na Nida kutokamilika.

Baadhi ya wafanyakazi ambao hawakutaka kutaja majina yao walisema genge hilo limefanikiwa kuwatapeli baadhi ya wafanyakazi ambao wanatarajia kustaafu katika utumishi wao wa umma.

Walisema mpaka sasa vyombo vya dola vimeshatoa tahadhari kwa wafanyakazi wote na kuwa kuna msako wa chini kwa chini unaendelea kuwabainia matapeli hao ambao wanadaiwa kupita katika halmashauri tofauti na kuwatapeli baadhi ya wafanyakazi kwa kutumia jina la Ofisi ya Rais Utumishi na Tamisemi ili kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

"Hawa matapeli wadai kuwa wafanyakazi wote wanaotarajia kustaafu na kuhama vituo vyao vya kazi na ambao taarifa zao haziko sawa wanatakiwa kutoa fedha ili waweze kuwasaidia haraka iwezekanavyo, hata hivyo kuna baadhi ya wafanyakazi wameshatapeliwa mpaka sasa," alisema mmoja wa wafanyakazi hao.

Genge hilo pia limedaiwa kutoa vitisho kwa baadhi ya wafanyakazi ambao wamekutana nao kuwa wakichelewa kutoa fedha ili waweze kufanya marekebisho ya taarifa zao wataondolewa kwenye mfumo wa malipo ya mishahara yao kazini.



# Rostam Azizi aimwagia Zanzibar vifaa vya mil. 500/- vita ya corona

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amepokea msaada wa vitu mbalimbali vyenye thamani ya Sh.milioni 500 kutoka kwa mfanyabiashara, Rostam Azizi.

Miongoni mwa vitu vilivyotolewa na mfanyabiashara huyo ni vitakasa mikono 3,000 kwa ajili ya wasafiri wa dalalala zote za hapa visiwani Zanzibar, barakoa 20,000, kifaa cha kumpatia mgonjwa oxygen, vifaa vya kupima mwenendo wa moyo na mashine ya kupumulia.

Mfanyabiashara huyo pia ametoa mashine kubwa ya senitizer kwa ajili ya Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja na mashine kubwa kama hiyo itawekwa katika Soko Kuu la darajani, Bandari ya Malindi ikiwa ni njia mojawapo ya kuzuia maambukizi ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19 Zanzibar. Kutokana na msaada huo, Makamu wa pili wa Rais amemshukuru Rostam kwa uzalendo wake na moyo wake wa kuisaidia jamii katika kipindi hiki ambacho vitu hivyo vinahitajika.

"Vita hii sio ya mtu mmoja, ni vita yetu sote, maana tunapigana na mtu ambae hatumuoni," alisema Balozi Iddi. Katika hatua nyingine, Makamo wa Pili wa Rais amewataka wananchi wa Zanzibar kuvaa barakoa na kuacha tabia ya ubishi kwa kutofuata maelekezo ya serikali na wataalam wa afya wanayoyatoa katika kipindi hiki.

"Sisi Zanzibar tunasemwa semwa sana kwa ukaidi, kwa hiyo sasa sio muda wa kufanya hayo, tuache ukaidi na tuvae barakoa, tujitahidi sana kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalamu wetu wa afya, "alishauri Makamu wa Rais.



Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohamed, akizungumza baada ya kuzindua picha maalum iliyochorwa na Seif Soud Ali, iliyobeba ujumbe 'Elimu ya watoto wetu ni jukumu letu sote'. Picha hiyo imedhaminiwa na Naibu Waziri huyo kwa Sh.400, 000. Hafla hiyo ilifanyika makao makuu ya Wizara ya Elimu, Mjini Zanzibar jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

## Mwanahabari aadhibiwa kisa habari corona

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WIZARA ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar kupitia Idara ya Habari (Maelezo), imemfungia mwaandishi wa habari wa gazeti la Tanzania Daima, Talib Ussi Hamad, kwa kutojishughulisha na shughuli yoyote ya uwandishi wa habari kwa muda wa miezi sita.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari juzi na kusainiwa na Mkurugenzi wa Maelezo Zanzibar, Dk. Juma Mohmmed Salum, mwaandishi huyo amekiuka maadili ya taaluma ya uandishi wa habari.

Alisema ,mwandishi huyo alisambaza taarifa za mgonjwa wa virusi vya corona bila ridhaa ya muhusika, na kuwa kitendo hucho ni kinyume cha sheria na utaratibu wa kitabibu.

Dk. Juma alisema kuwa Idara ya Habari imetoa adhabu kwa mwandishi huyo kwa kutumia kifungu cha 41,42(a) na (b) cha Sheria ya Magazeti, Vitabu na Wakala wa Habari Namba 5 ya mwaka 1988 na marekebisho yake Namba 8,ya mwaka 1997.

Alisema kwa kutumia vifungu hivyo vya sheria, mwaandishi huyo haruhusiwi kukusanya, kusambaza na kufanya shughuli yoyote ya uwandishi wa habari kwa kipindi cha miezi sita.

# Wagonjwa wapya wa corona Unguja 11, Pemba watano

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar, imetoa taarifa ya ongezeko la wagonjwa wapya 16 wa virusi vya corona hapa nchini na kufikia idadi ya wagonjwa 74 kutoka wagonjwa 58 ambapo walitangazwa hapo awali Aprili 19, 2020. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Wizara ya Afya na kusainiwa na Waziri wa Afya Zanzibar Hamad Rashidi juzi, kati ya wagonjwa hao wapya wagonjwa 11 wanatoka kisiwa cha Unguja na wagonjwa watano wanatokea Kisiwa cha Pemba. Taarifa hiyo ilisema kuwa kati ya wagonjwa hao 16, wagonjwa 15 ni raia wa Tanzania na mgonjwa mmoja raia wa Tanzania.

Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kuwasisitiza wananchi kuchukua taathari zote za kujikinga na ugonjwa huo zinazotolewa mara kwa mara ikiwamo unawaji mikono kwa maji ya kutiririka kwa kutumia sabuni, kujiepusha misongamano, kuahirisha safari za ndani na nje ya nchi zisiso na ulazima.

Taarifa hiyo pia imesisitiza wananchi wa visiwa vya Zanzibar kuvaa barakoa muda wote wanapotoka nje ya nyumba zao ambapo pia serikali itatoa maelekezo ya namna ya uvaaji wa barakoa hizo pamoja na aina inayotakiwa kuvaliwa.

Kadhalika, serikali kupitia Wizara ya Afya Zanzibar, imewaomba wananchi ambao wanadalili za homa kali, kukohoa na kupiga chafya kujitokeza katika vituo vya afya au kupiga simu kwa namba ambazo zimetolewa kwa ajili ya kupata msaada.

Hata hivyo, Wizara ya Afya imeendelea kuvisisitiza vyombo vya habari kupata taarifa za ugonjwa wa corona kutoka kwa Wizara hiyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**MOHSIN HENRY MSUYA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1071-0374** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ST MATTHEW SEKONDARI mwaka 2004. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MBU/RB/327309/2020.**

115710602

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

**'WAMILIKI WA KAMPUNI YA THE SHIMMER LIMITED** (NAMBA YA USAJILI **131069** YA TAREHE10/11/2016 WANAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA KAMPUNI YAO TANGIA IMEFUNGULIWA HAIKUWA NA MUENDELEZO WOWOTE, HIVYO WAMEAMUA KUIFUNGA KWA MUJIBU WA SHERIA YA MAKAMPUNI BRELA'

115711302

## TANGAZO LA KUPOTEA KWA OFFA YA KIWANJA

**KANONI JONAS CHOMA** MKAZI WA NDEMBEZI MANISPAA YA SHINYANGA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFFA YA KIWANJA NAMBA 30 KITALU "Z"IBINZAMATA MANISPAA YA SHINYANGA AMBAYO ILIPOTEA MWAKA 2014 MAENEO YA IBINZAMATA SHINYANGA KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA KANONI JONAS CHOMA KWA SIMU NAMBA **0763161715 AU 0764993759.**
**RB NAMBA SHY/RB/2020,**
**CONTROL NAMBA 9910812347595.**

115710702

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FADHILI SAIDI MDEMO** Amepotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA NOAH.Yenye usajili wa namba T 496 DDR.Yenye chasis namba SR5000061220 na injini namba 35.

Yeyote atakaeiona anaomba atoe taarifa Kituo chochote cha polisi.

RB namba MOR/MOR/RB/323968/2020.

115710402

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF TANZANIA**
**AT ARUSHA**
**CIVIL/APPEAL/CASE NO. 82 OF 2015**
**HAIKA BENSON MAWALA PLAINTIFF/APPELLANT**
**VERSUS**
**EMIL NELSON ANDREA DEFENDANT /RESPONDENT**
**NOTICE OF HEARING/MENTION**

**TO EMIL NELSON ANDREA**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention/hearing in the Resident Magistrate's Court of Arusha at Arusha on the 23rd day of APRIL 2020 at 08:30 am o'clock in the forenoon.

You may appear in person or by Advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTICE** that in default of your appearance on that day time before mention or hearing the Court may proceed in your absence.

Given under my hand and the seal of the court this 16th day **of APRIL 2020.**

RESIDENT MAGISTRATE
ARUSHA

115711202

## KUPOTEA KWA PASSPORT YA KUSAFIRIA



**SEIF PEMBE SELEMAN** anatangaza kupotelewa Passport ya kusafiria yenye namba **TAE 269019,** kwa yeyote atakaeona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu au ofisi ya idara ya uhamiaji. Taarifa Polisi **SO/RB/1726/2020 Au apige simu namba: 0748173893**

115710902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JAMES SHAFRAEL MANGIA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 783 ATA MITSUBISHI CANTER.** Chassis namba **FE52CE450160.** Engine namba **4D33H12699.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/319449/2020.**

115710502

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ABDALLAH RAMADHAN SALUM** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 632 CBR.** Chassis namba **LD3PCK6J2J2006577.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DSM/PHQ/RB/312071/2020.**

115711102

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LUCAS KAYOBYO SHEMU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 548 DJW TOYOTA CROWN. Chassis namba GRS1805006178. Engine namba 4GR0018061.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/324195/2020.**

157102

## KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA

DAR ES SALAAM
UTHIBITISHO WA USIMAMIZI MIRATHI
MIRATHI Na. 75 ya mwaka 2019
MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU
KOHELETHY KAINJA MARGAI
MWOMBAJI/WAOMBAJI
PIERRE EDWALD MAREGESI MARGAI
TAARIFA YA KAWAIDA
(KANUNI YA 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu alietajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika Jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 5 mwezi wa Mei 2020@ 5:00 asubuhi.

Imewasilishwa Dar es Salaam, leo tarehe 9 mwezi wa April 2020.

NAIBU MSAJILI

NAKALA KWA:
PIERE E.M MARGAI,
P.O BOX 16210
D'SALAAM

157099

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Bibi wa miaka 68 ajifungua mapacha

**LAGOS,** Nigeria

MWANAMKE mwenye miaka 68 nchini Nigeria, amejifungua watoto pacha na kuwaacha watu wakishangaa.

Bibi huyo alijifungua katika Hospitali ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Lagos.

Akitoa tangazo hilo jumapili, Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la chuo hicho, Prof. Wasiu Adeyemo, alisema kuwa mwanamke huyo alijifungua kwa njia ya upasuaji baada ya wiki 37 za ujauzito.

Mume wa mwanamke huyo, Noah Adenuga, alisema iliwachukua muda wa miaka 43 kutafuta mtoto, kwamba waliwahi hata kutumia njia ya kuanguliwa kwa mayai yake ya uzazi nje ya mfuko wa uzazi na baadae kuchanganywa na mbegu za kiume na kisha kupandikizwa ndani ya mfuko wake wa uzazi (IVF).

**Daktari aliyemuhudumia mama huyo, Adeyemi Okunowo, alitaja kuzaliwa kwa watoto hao ni muujiza.**

Alisema lakini hawakufanikiwa kupata mtoto licha ya kutumia njia hiyo. Alisema hata wakati huu mafaniko yao yamepitia njia hiyo ya IVF.

Mama huyo na watoto wake wachanga wanaendelea vizuri na kwa sasa wameruhusiwa kutoka hospitalini na kurudi nyumbani kwake.

Adenuga alisema safari yao ya kutafuta watoto iliwapeleka hadi nchini Uingereza na kuwarejesha tena Nigeria, imani yao iliwafanya waendelea kuishi pamoja kwa miaka mingi bila watoto.

Adenuga mwenye umri wa miaka 70, alisema alipokea jumbe kutoka kwa kikundi cha madaktari wa uzazi ambao walisema matendo yake ni ya kijinga.

Daktari aliyemuhudumia mama huyo, Adeyemi Okunowo, alitaja kuzaliwa kwa watoto hao ni muujiza.

Alisema mume huyo na mke wake walijiweka hatarini kwa kuamua kusaka mtoto katika umri wao mkubwa.

Utawala wa hospitali hiyo ulisema kuwa usingewapatia huduma ya IVF katika umri wa miaka 68, lakini waliamua kumtibu kwa sababu ulikua ni wajibu wao wa kimatibabu.

Walisema siyo mara ya kwanza kwa mwanamke kikongwe kujifungua.

Mwanamke mwingine nchini India, Mangayamma Yaramati, alijifungua Septemba mwaka jana watoto pacha akiwa na miaka 73 katika jimbo la Kusini la Andhra Pradesh baada ya kutungishwa mimba kupitia njia ya IVF.

Mangayamma Yaramati alisema kuwa yeye na mumewe ambaye alikua na umri wa miaka 82, muda wote walikuwa wakitafuta watoto lakini hawakuwahi kufanikiwa hadi walipotumia njia ya IVF.

"Tulijaribu mara nyingi kupata watoto na tukawatembelea madaktari wengi, kwa hiyo hiki ni kipindi cha furaha zaidi maishani mwangu ." alisema Yaramati **BBC**

## Rais Trump kuwapiga 'stop' wahamiaji

**NEWYORK,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump ametangaza kuwa atasaini amri ya kuzuia kwa muda aina zote za uhamiaji nchini humo ili kupambana na virusi vya corona .

Katika ujumbe alioutoa katika mtandao wa kijamii wa Twitter, Rais Trump alieleza kile alichokitaja kama shambulio la adui asiyeonekana, kama anavyoviita virusi vya corona, pamoja na haja ya kulinda kazi za raia wa Marekani.

Hata hivyo, haijafahamika kufikia sasa ni programu gani za uhamiaji ambazo zitaathirika, wakosoaji wake wanadai kuwa Rais Trump anatumia janga la corona kuwafungia milango wahamiaji.

Hali hiyo inakuja wakati ikulu ya Marekani ikisema pia kwamba janga baya zaidi la virusi vya corona limepungua na shughuli zinaweza kuanza kufunguliwa nchini humo.

Marekani tayari imekubaliana na Canada pamoja na Mexico kuongeza zaidi muda wa kuzuia safari zisizo na muhimu baina ya mipaka yao, hadi katikati ya mwezi mei.

Safari pia zimezuiwa kwa kiwango kikubwa kwa watu wanaotoka Ulaya na China kuelekea Marekani, ingawa watu wenye vibali vya kazi vya muda, wanafunzi na wafanyabiashara wanaruhusiwa.

Tangazo hilo la Rais Trump linakuja wakati utawala ukitaka shughuli zifunguliwe katika baadhi ya maeneo ya nchi hiyo ambako zilikuwa zimefungwa kutokana na janga la corona.

Juhudi za Rais Trump za uongozi kwa mitandao ya habari ya kijamii zinapaswa kuchukuliwa kwa kiasi fulani kama sehemu ya ukweli.

Taarifa juu ya marufuku ya muda kuhusu uhamiaji wa aina zote ilitangazwa saa chache kabla ya saa sita za usiku siku ya Jumatatu na kutoa mwangaza zaidi juu ya hatua na uhalali wa kisheria wa maamuzi yake.

Lakini bado kuna wasiwasi kwamba kwa namna yoyote ile hatua hiyo itapingwa vikali na makundi yanayounga mkono uhamiaji, wenye maslahi ya kibiashara na wanaopinga fikra za Rais Trump.**BBC**



Wanaanga, Jessica Meir (kushoto), Andrew Morgan (katikati) wa Shirika la Marekani la anga za Juu (NASA), pamoja na Oleg Skripochka wa Urusi wakiwasili duniani baada ya kukaa siku 200 katika anga za mbali. **PICHA: REUTERS**

## Rais ajiweka karantini kisa mlinzi

**FREE TOWN,** Sierra Leone

RAIS wa Sierra Leone, Julius Maada Bio, amejiweka karantini siku 14 baada ya mmoja wa walinzi wake kukutwa ameambukizwa virusi vya ugonjwa wa corona.

Rais Bio alitangaza siku ya Jumatatu usiku kuwa ana afya njema ingawa mfanyakazi wake ana maambukizi ya ugonjwa huo.

Alisema familia yake iko salama na hakuna aliyeonesha dalili za kuwa na maambukizi ya virusi hivyo.

Alisema atakaa karantini kwa siku 14 kwasababu alikuwa karibu na mlinzi wake.

Mwanzoni mwa Aprili, mwaka huu, Botswana ilisema kuwa inamuweka karantini Rais wa nchi hiyo Mokgweetsi Masisi pamoja na baadhi ya wabunge, baada ya muuguzi ambaye alikuwa kwenye kikao maalumu cha bunge kukutwa na maambukizi ya virusi vya corona.

Kikao hicho maalumu kiliitishwa na Rais Mokgweetsi Masisi kutaka idhini ya kutangazwa hali ya hatari kwa miezi sita, kupambana na maambukizi ya virusi vya corona.

Lakini wabunge walishtushwa baada ya kugundua kuwa mhudumu wa afya aliyekuwa akiwapima virusi vya corona siku moja kabla alikutwa na maambukizi ya ugonjwa huo.

Rais Masisi alijitenga kwa siku 14 mwezi uliopita baada ya kusafiri kwenda nchi jirani ya Namibia.

Katika kisa kingine cha aina hiyo, msaidizi mkuu wa Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari alikutwa na virusi vya corona.

Abba Kyari, akiwa na umri wa miaka ya 70 alikuwa mtu muhimu kwa Rais Buhari na serikali yake kwa ujumla.

Siku ya Jumamosi, ofisi ya Rais Buhari Ilitangaza kifo cha Abba Kyari, mzee huyo alikuwa na historia ya maradhi mengine kama kisukari. **BBC**

# NAPOLI YAKUBALI KUMUUZA KOULIBALY



**NAPLES,** Italia

KLABU ya Napoli imesema ipo tayari kumuuza mlinzi wake wa kati, Kalidou Koulibaly, ambaye ni raia wa Senegal wakati wa dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto.

Koulibaly amekuwa akitajwa sana kuwaniwa na klabu ya Manchester United ya England na sasa huweza akatua pale kwenye dimba la Old Trafford.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, klabu yake ya sasa ipo tayari kumuuza kwa dau lisilopungua pauni milioni 74, hivyo United ina nafasi ya kumsajili kwenye dirisha la usajili lijalo.

Mwenyekiti wa klabu ya Napoli, Aurelio De Laurentiis inadaiwa amekubali kuumuza beki huyo wa kimataifa wa Senegal.

Kwa muda mrefu sasa, Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer, amekuwa akidaiwa kumhitaji Koulibaly ili akaujenge ukuta wake.

Beki huyo bado ana mkataba ndani ya Napoli hadi mwaka 2023, lakini kukubali kwa kigogo wa klabu hiyo kumuuza ina maana wakati wowote anaweza kuondoka klabu hapo.

Pia klabu za PSG na Manchester City zimekuwa zinampigia hesabu beki huyo mwenye urefu wa futi 6 na inchi 1.

# Haaland asubiriwa Real Madrid

**MADRID,** Hispania

MSHAMBULIAJI nyota wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland, kwa sasa anahesabiwa siku tu kabla ya kutua kule Real Madrid.

Madrid inamfukuzia Haaland, ikiwa haitaki kufanya kosa kama ilivyokuwa dirisha lililopita alipodakwa na Wajerumani kutoka klabu yake ya RB Salzburg.

Fowadi huyo anatajwa kusakwa pia na Manchester United na Barcelona na duru za kispoti zinasema kuwa Madrid wanamtaka kwa udi na uvumba ili kuimarisha safu yao ya mbele ambayo imepoteza makali tangu, Cristiano Ronaldo atimkie Juventus, huku Gareth Bale akisumbuliwa na majeruhi na pia kutoiva na Kocha, Zinedine Zidane.

Taarifa zaidi zinasema Real Madrid inamtumia raia mwenzake wa Norway, Matrin Odegaard, anayekipiga Santiago Bernabeu kwa mkopo kutoka Real Sociedad ili kumvuta mkali huyo.

Mchezaji huyo amekuwa na msimu mzuri zaidi ambapo hadi sasa amefunga mabao 40 katika klabu mbili za Salzburg na Dortmund.





# *Wachezaji Arsenal wakubali kukatwa mishahara*

**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal imetangaza wachezaji wake wamekubali kukatwa asilimia 12.5 ya mishahara yao, baada ya kuahidiwa 'bonasi' kubwa wakifuzu kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana kupitia tovuti yake imesema wachezaji watafidia fedha watakazokatwa kwa kila mmoja kulipwa pauni 100,000, endapo watafuzu msimu ujao kucheza Ligi ya Mabingwa ya Ulaya.

Klabu pia, imeahidi kumlipa kila mchezaji bonasi ya pauni 500,000 kama watatwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2021 au pauni 100,000 kama wataibuka Mabingwa wa Ligi ya Europa.

Arsenal, imekuwa klabu ya kwanza ya Ligi Kuu England, kukubali mpango wa kukata mishahara kwa wachezaji wake, katika kipindi hiki ambacho klabu nyingi duniani zimeathirika kiuchumi kutokana na janga la virusi vya corona.

Arteta amesema kwamba, wachezaji wake kwa kauli moja wamekubali kukatwa mishahara yao ili kuwasaidia wafanyakazi wengine wa klabuni hapo.

"Ndio wote wamekubali na wanataka mishahara hayo kwa asilimia 12.5 kusaidia kuwalipa wafanyakazi wengine ndani ya klabu," ilisema taarifa ya Arsenal.

HABARI MICHEZO

# Neuer kusaini mkataba mpya Bayern

**MUNICH,** Ujerumani

OFISA Mtendaji wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge, anaamini, Manuel Neuer ataongeza mkataba na klabu hiyo.

Golikipa huyo mwenye umri wa miaka 34 mkataba wake wasasa unamalizika msimu wa 2020-21 huku bado kukiwa hakuna mazungumzo kwa ajili ya kuongeza mkataba mpya.

Kumekuwa na ripoti kwamba, Neuer anataka mkataba wa miaka mitano wenye thamani ya euro milioni 20 kwa mwaka, lakini alikanusha taarifa hizo wakati wa mahojiano yake na gazeti la Bild.

Neuer pia ameweka wazi kwamba hana furaha na namna majadiliano yake ya mkataba mpya yalivyovuja kwenye vyombo vya habari.

Hata hivyo, Rummenigge, anajiamini kwamba pande zote mbili zitaelewana na kufikia makubaliano kuwa golikipa huyo Mjerumani kubakia pale kwenye dimba la Allianz Arena.

"Wote tunajua nini tulichonacho," alisema akiliambia gazeti la Bild Jumatatu.

"Na kwa hali jinsi ilivyo, nina uhakika kwamba tutapata suhulu mwishoni na Manuel Neuer atasaini mkataba mpya.

"Tuna golikipa bora duniani na tayari tumeshinda kila kitu tukiwa naye."





# MATA: HAZARD NDIO MCHEZAJI WANGU BORA EPL

**MADRID,** Hispania

KIUNGO wa Manchester United, Juan Mata, amesema kwamba, Eden Hazard ni jina la kwanza linalojitokeza kwenye akili yake anapoulizwa kuhusu mchezaji bora zaidi kuwahi kucheza kwenye Ligi Kuu England.

Mata, anaamini mchezaji mwenzake huyo waliyewahi kuwa pamoja kule Chelsea, atafikia mafanikio makubwa kwenye kikosi cha Real Madrid na kinamchotokea kwa sasa ni mapito tu.

Mata na Hazard walicheza pamoja kwa msimu mmoja na nusu pale Stamford Bridge kabla ya raia huyo wa Hispania kutimkia United, Januari 2014, lakini miezi hiyo 18 ilitosha kutambua uwezo wa nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji.

"Mchezaji bora kwenye Ligi Kuu England? Nina maana yule niliyependa kucheza naye timu moja au timu pinzani, ni Eden Hazard," alisema Mata akinukuliwa na Sky Sport.

"Kwangu mimi, kwa miaka mingi, alikuwa mchezaji bora kwenye ligi. Anaweza kushinda mechi kwa uwezo wake binafsi. Nilikuwa nafanya naye mazoezi, hivyo nafahamu ni mzuri kiasi gani.

Alisema amekosa tu bahati kwenye maisha yake mapya huko Real Madrid kutokana na kuwa majeruhi, lakini anajua atawaonyesha ubora wake na wote wataona wakati atakapokuwa fiti.

# *Newcastle yakaribia kuuzwa*

**NEWCASTLE,** England

KAMPUNI ya Saudia Arabia ya Public Investment Fund chini ya Mfalme Mohammed Bin Salman, ipo tayari kuinunua klabu ya Newcastle United, kwa kiasi cha euro milioni 300 kutoka kwa mmiliki wake, Mike Ashley.

Kampuni hiyo, imefanya mkutano na waandishi wa habari na kuweka malengo yake baada ya kuinunua klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu England.

"Tumefikia pazuri na mmiliki wa klabu ya Newcastle United wa sasa, Mike Ashley, kuwa atatuuzia huku kuna baadhi ya mambo tunaendelea kuweka sawa. Malengo yetu makubwa ni kuifanya kuwa timu yenye ushindani kwenye Ligi Kuu England na Ulaya," ilisema taarifa ya mfalme huyo.

Taarifa hiyo iliongeza; "Sisi ni mashabiki wakubwa wa Newcastle United, tulikuwa tunaifuatilia mwendo wake kwenye Ligi Kuu England, tunahitaji kuwa tishio kama Chelsea chini ya Roman Abramovich na Manchester City chini ya Sheikh Mansour.

"Tuna ndoto za kushinda Ligi Kuu England pamoja na michuano mikubwa Ulaya na hilo linawezekana.

"Mwaka 2019 nilikuwa nataka niinunue klabu ya Manchester United, nilikuwa nipo tayari kuinunua kwa kiasi cha euro bilioni 3.8, lakini familia ya Malcom Glazer ilikuwa inataka euro bilioni 4.9.

"Tunataka kuwasajili wachezaji wakubwa Ulaya, makocha bora waje kuleta mapinduzi kwenye timu yetu, tunataka kupanua uwanja na tunaweza tukaendelea kutumia jina la St James Park au kubadilisha jina."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RASHFORD AMSHUKURU MOURINHO KUMJENGA

## ●●● Lakini aeleza alikuwa na kipindi kigumu chini ya Mreno huyo ambaye aliinoa United...

**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI, Marcus Rashford, amekiri alikuwa na 'kipindi kigumu' ndani ya kikosi cha Manchester United kilipokuwa chini ya Jose Mourinho, lakini kocha huyo Mreno alimjenga kiakili.

**Mourinho aliiongoza United kuanzia majira ya joto mwaka 2016 hadi Desemba 2018, na alishinda taji la Ligi ya Europa na Kombe la Ligi mwaka 2017.**

Katika kipindi hicho akiwa United, Mourinho alikosolewa zaidi kutokana na aina ya uchezaji ambayo timu hiyo ilikuwa inacheza, wakati huo huo akiwa hapatani na wachezaji tegemeo kama Paul Pogba.

Rashford alifunga mabao 28 na kutoa pasi za mwisho za magoli 20 chini ya Mourinho, ambaye kwa sasa ni kocha wa Tottenham.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 22 amefunguka licha ya kupata changamoto hiyo chini ya Mourinho, lakini anakiri alipata uzoefu zaidi na nafasi kubwa kiwango chake kuimarika tofauti na alivyokuwa kabla ya kutua kwa kocha huyo.

Rashford aliuambia mtandao rasmi wa Manchester United: "Ulikuwa ni wakati mgumu lakini nafikiri nikirudi nyuma miaka mitano au sita ninaweza kukumbuka kwamba ilikuwa ni wakati wenye changamoto zaidi.

"Kama mchezaji wa kila siku ninayejifunza, nimeimarika kwa kiasi kikubwa na nilipata pia wakati mgumu kwa muda wa miaka miwili niliyokuwa chini ya Jose. Tulikuwa na kupanda na kushuka, ninapoangalia nyuma, nilikuwa na wakati mgumu lakini kwa hakika kipindi hiko kilinijenga kuwa mchezaji mzuri."

Mourinho alipenda kumweka nje ya kikosi chake Rashford, na nyota huyo wa Timu ya Taifa ya England alitumia muda huo kujifunza na alimtengeneza kujiamini zaidi.

Chini ya Mourinho, Rashford alifanya madhambi mengi zaidi kuliko wakati mwingine na ilisababisha aonyeshwe kadi 13 za njano pamoja na kadi moja nyekundu.

Tangu Mourinho alipoondoka katika timu hiyo, Rashford ameonekana kuimarika zaidi na chini ya Kocha Ole Gunnar Solskjaer, amefunga mabao 19 kwenye mechi 31 alizoichezea United msimu huu.

## ZISIKUPITE

### CORONA YAMGUSA KANE

MANCHESTER United haitaweza kununua mchezaji ghali kama straika wa Spurs, Harry Kane (26), huku ikifikiria mipango ya kukiimarisha zaidi kikosi chake katika dirisha la usajili wakati pia hali ya kifedha ikiathiriwa na kuwapo na maambukizi ya virusi vya corona. ***(Guardian)***

### SANCHO, KANE SOKONI

MABOSI wa Manchester sasa imewaweka katika orodha ya nyota inaowahita straika wa Spurs, Harry Kane na winga wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho ambaye ana umri wa miaka 20. ***(Evening Standard)***

### SOUNESS AIONYA UNITED

KIUNGO wa zamani wa Liverpool na Mchambuzi wa Soka, Graeme Souness ameionya Manchester United uamuzi wake wa kumsajili winga Jadon Sancho utaweweka kwenye wakati mgumu dhidi ya klabu yake ya Dortmund. ***(Daily Mirror)***

### MBAPPE ASHUKA THAMANI

DAU la kumuuza mshambuliaji wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe (21), ambalo limetajwa kuwa ni pauni milioni 250, kuelekea Real Madrid linaweza kupungua kwa pauni milioni 35 kwa sababu ya kuwapo kwa kesi ya virusi vya ugonjwa wa corona, amesema mmoja wa wajumbe wa Bunge la Ulaya. ***(Daily Mirror)***

### ATLETICO YAMGANDA PARTEY

KIUNGO wa Atletico Madrid, Mghana Thomas Partey (26), ambaye anawindwa na Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, klabu yake hiyo ya Hispania inaamini inaweza ikafanikiwa kumpa mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia timu hiyo. ***(Express)***

### AUBAMEYANG ANUKIA CITY

MANCHESTER City imeingia kwenye mbio za kuwania saini ya straika wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang, huku Barcelona, Inter Milan na Real Madrid pia zinatajwa kuwinda saini ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 30, na ambaye anamaliza mkataba wake na klabu hiyo kipindi cha majira ya joto mwakani. ***(Express)***

### UNITED YABADILI GIA

MANCHESTER United imejiondoa kwenye mbio za kuwania saini ya kiungo wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Colombia, James Rodriguez (28), lakini Arsenal na Everton zenyewe bado zinamwania nyota huyo. ***(Sky Sports, via the Sun)***

### SILVA, VALENCIA WATETA

KIUNGO wa Manchester City, David Silva (34), yuko katika mazungumzo na klabu yake ya zamani ya Valencia baada ya mkataba wake wa sasa kumalizika ifikapo Juni 30, mwaka huu lakini mazungumzo hayo yamesimama kutokana na kuwapo kwa ugonjwa wa corona. ***(ESPN, via Manchester Evening News)***

### PSG KUIBOMOA PORTO

VIGOGO wa Ufaransa, Paris St-Germain, wanajiandaa kumnunua mchezaji mmoja kutoka Porto kwa dau la pauni milioni 21.8m. ***(Gauchazh, via the Sun)***

### CHELSEA KUMKOSA TELLES

CHELSEA inajiandaa kumkosa beki wake, Alex Telles, lakini inajiimarisha kuweka nguvu kuwania saini ya, Ben Chilwell wa Leicester. ***(Gauchazh, via the Sun)***

HABARI MICHEZO

## Miquissone aitaja Biashara United

**Na Mwandishi Wetu**

WINGA mpya wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, Luis Miquissone, amesema bao lake la kwanza kufunga akiwa na timu hiyo ndio goli pekee analolifurahia zaidi.

Miquuisson alifunga bao la kwanza katika mechi dhidi ya Biashara United ambapo Simba iliondoka na pointi tatu.

Mchezaji huyo wa kimataifa kutoka Msumbiji alifunga bao hilo akimalizia kazi nzuri kutoka kwa kiungo mkongwe, Jonas Mkude.

"Naweza kusema bao langu bora ndani ya Simba ni bao langu la kwanza, kwa sababu lilinifanya kuwa na furaha kubwa, ndio lilikuwa katika changamoto yangu mpya," alisema nyota huyo wa zamani wa UD Songo.

Aliongeza bao hilo halitaondoka katika historia yake na anaamini ataendelea kuisaidia Simba kupata matokeo bora zaidi katika Ligi Kuu Bara na mashindano yote watakayoshiriki.

Hadi Ligi Kuu Bara inasimama, Simba ndio walikuwa vinara katika msimamo baada ya kujikusanyia pointi 71.

## Mipango yasukwa kuinusuru Ndanda

**Na Saada Akida**

TUTABAKI! Kocha Mkuu wa Ndanda FC, Abdul Mingange, amesema ameandaa mpango 'kabambe' ya kuhakikisha timu hiyo ya mkoani Mtwara inabakia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Mingange aliliambia gazeti hili kipindi hiki amewapa wachezaji wake mbinu mpya za mazoezi na anawafuatilia ili kuhakikisha wanayafanyia kazi katika kipindi hiki cha maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Kocha huyo (pichani chini) alisema mbali na mbinu hizo amekuwa pia akitenga muda maalum kwa kuzungumza na wachezaji wake ili kuwajenga zaidi kisaikolojia.

"Nimeikuta Ndanda katika hali mbaya ya kushuka daraja, nikawaandaa kisaikolojia hadi sasa kufika nafasi ya 16, tulipo pia sio salama, tunatakiwa kufanya vizuri mechi zilizobakia, ninawahimiza kuzingatia mazoezi," alisema Mingange.

Aliongeza mbali na kuwapa mbinu pia amekuwa akisisitiza juu ya kujali kazi yao kwa kupambana ili timu hiyo iendelee kubakia katika Ligi Kuu Bara msimu ujao.

"Ninachowaambia kila siku ni kuzingatia mazoezi ili tutakaporejea katika ligi, tuwe imara, lakini wachezaji wanatakiwa kutambua timu itakaposhuka basi tutashuka chini kuanza upya mapambano," alisema kocha huyo.



# BEKI COASTAL AFUNGUKA 'ANAVYOMUOTA' KAGERE

**Na Saada Akida**

WAKATI Ligi Kuu ikiwa bado imesimama, beki tegemeo wa Coastal Union ya jijini Tanga, Bakari Mwamnyeto, amemtaja Meddie Kagere wa Simba ndiye mshambuliaji pekee 'anayemuumiza kichwa' katika ligi hiyo ya juu hapa Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwamnyeto alisema amekuwa na wakati mgumu pale anapomkaba straika huyo na analazimika kuongeza umakini ili kulinda lango lake.

Mwamnyeto alisema Kagere amekuwa na 'uchu' wa kufunga magoli na pia ni mshambuliaji anayetumia akili na nguvu kuhakikisha anaisaidia timu yake.

**"Kuna washambuliaji wengi wazuri ila Kagere amekuwa anahitaji kufunga muda wote, hivyo unatakiwa kumchunga na kutumia akili ili asilete madhara katika timu yako," alisema beki huyo ambaye ni shabiki wa Liverpool ya England.**

Nahodha huyo wa Coastal Union alisema licha ya kumpa wakati mgumu, alifanikiwa kumkaba vema alipokuwa kwenye majukumu ya Taifa yeye akiwa na Taifa Stars na kinara huyo wa mabao nchini akiwa kwenye kikosi cha Rwanda (Amavubi).

Mwamnyeto alisema ukiondoa nyota huyo, kwa sasa hakuna mshambuliaji mwingine ambaye anamsumbua licha ya baadhi yao kuwa na majina na sifa 'lukuki'.

Beki huyo ambaye ni tegemeo ndani ya kikosi cha Coastal Union ndiye mchezaji ghali kwa nyota wazawa na tayari yuko kwenye rada za vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga.

Meneja wa mchezaji huyo anadai ili kumng'oa jijini Tanga, klabu inayomhitaji itatakiwa kutoa kiasi cha Sh. milioni 240.




Wachezaji wa Yanga wakiwa katika picha ya pamoja kabla ya kupokea vifaa vya michezo vilivyotolewa na Kampuni ya GSM, kwa ajili ya kufanyia mazoezi binafsi katika kipindi hiki cha kujikinga na virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19). **PICHA: MTANDAO**

# Corona yakitesa kikosi cha wavu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Timu ya mpira wa mikono ya Tanzania, Kombo Ally Kombo, amesema kuahirishwa kwa michuano ya Kombe la Chalenji kumekiathiri kikosi chake kwa sababu wachezaji wake walikuwa 'wameiva' na wako tayari kushindana.

Michuano ya Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati ilipangwa kufanyika Machi, mwaka huu nchini Ethiopia kwa wachezaji wa umri chini ya miaka 20 na 17, iliahirishwa kwa sababu ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa Corona.

Kombo aliliambia gazeti hili wachezaji wake walianza kwa muda mrefu na aliamini watakwenda katika michuano hiyo kushindana na si kusindikiza.

Kocha huyo alisema tayari aliwaruhusu wachezaji wake wanaotoka mikoa ya Tanzania Bara na Kisiwani Pemba wamesharejesha makwao baada ya kupokea taarifa za kuharishwa kwa michuano hiyo.

"Kikosi chetu tulikiandaa mapema mno, na wachezaji walikuwa na matumaini makubwa ya kwenda kufanya vizuri, lakini kuahirishwa kwa michuano hii katika hatua za mwisho kumewavunja moyo," alisema Kombo.

Kocha huyo amewataka wachezaji wake kuendelea na programu za mazoezi binafsi na kusubiri taarifa nyingine mpya kutoka kwa waandaaji wa michuano hiyo ya Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

# Michezo

Jumatano Aprili 22, 2020

Nipashe




Rashford amshukuru Mourinho kumjenga UKURASA 22



Kiungo wa Simba, Said Ndemla (katikati), ambaye anawindwa na klabu mbalimbali za hapa nchini, akiwa kwenye mazoezi na nyota wenzake wa Wekundu wa Msimbazi, Erasto Nyoni (kushoto) na Meddie Kagere. **PICHA : MAKTABA**

## Cheche achambua inapokwama Azam FC Bara

**Na Somoe Ng'itu**

ALIYEKUWA Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Nassor 'Cheche', amesema sababu mojawapo inayowafanya mabingwa hao watetezi wa mashindano ya Kombe la FA kushindwa kutwaa tena ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara nyingine ni kukosa uvumilivu.

Azam FC imetwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara mara moja katika msimu wa 2013/14, ikiwa chini ya Kocha Mkuu raia wa Uingereza, Stewart Hall.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Cheche alisema timu hiyo imeshindwa kuvumilia makocha wake na kuamia kuwatimua ndani ya muda mfupi baada ya kuona malengo yao hayatimii.

Cheche alisema mabosi hawapaswi kuangalia ubingwa peke yake na wanatakiwa kufuatilia maendeleo mengine yaliyoletwa na kikosi chao katika kila msimu.

"Shida ipo sehemu moja, hawana uvumilivu, ni lazima wafahamu hamwezi wote kuwa mabingwa, timu zinashindana, lakini mwisho wa siku bingwa anakuwa mmoja," alisema Cheche.

Kocha huyo lakini moja ya malengo mengine ya kuanzishwa kwa timu hiyo yalikuwa ni kuleta mapinduzi katika soka la hapa nchini na hakika hilo walifanikiwa. Aliongeza safari ya wachezaji wa Tanzania bado imekuwa na changamoto kwa baadhi yake kupewa sifa ambazo hazistahili na hili linachangia kurudisha nyuma maendeleo ya mchezo husika.

"Promo zimekuwa nyingi sana kuliko uhalisia, utakuta mchezaji amefanya tukio moja, basi litaelezea kila siku, tunawapandisha vichwa, tunawapa sifa sana, tunawamaliza na hatuwajengi," Cheche alisisitiza.

Mapema Machi, mwaka huu uongozi wa Azam FC iliamua kumpa majukumu mengine kwenye kampuni yao baada ya kudumu nayo kwa zaidi ya miaka 15.

# Vita ya viungo yakolea Yanga

### Kocha Mbelgiji afunguka ubora wa kiungo anayemhitaji, huku Ndemla akisisitiza safari...

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, bado anasaka kiungo mkabaji kwa ajili ya kuboresha kikosi chake, kiungo, Said Ndemla, amesisitiza hafikirii kujiunga na klabu nyingine ya hapa nchini endapo ataondoka kwa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba.

**Akizungumza na gazeti hili, Ndemla alisema bado anatamani kubakia Simba, lakini kama ni kuondoka, basi ataenda kucheza soka la kulipwa.**

Ndemla ambaye amekosa namba ya kudumu katika kikosi cha Simba, amesema anaamini huu ni wakati sahihi wa kwenda kucheza soka Ulaya na tayari ameshaanza mazungumzo na klabu zinazowania saini yake za ndani na nje ya Tanzania.

"Bado natamani kuendelea kubaki ndani ya klabu ya Simba baada ya mkataba wangu kumalizika mwishoni mwa msimu huu, nimepata ofa mbalimbali za klabu za Tanzania, ila natamani kucheza nje ya nchi, ndiyo ndoto yangu," alisema Ndemla.

Eymael aliliambia gazeti hili amepewa jukumu la usajili na kusema tayari ameanza kufanya mazungumzo na kiungo mkabaji mmoja kwa ajili ya kupata saini yake.

Hata hivyo kocha huyo hakutaka kuweka wazi ni mchezaji gani ambaye yuko katika 'rada' zake na kuongeza mipango yake ni kuunda kikosi cha ushindani.

" Ninaendelea na mazungumzo, ninahitaji kupata kiungo mmoja mkabaji wa kimataifa atakayecheza namba sita, nina upungufu katika eneo hilo, nina imani na uwezo wa viungo nilionao Yanga, lakini ni lazima nisajili kiungo mmoja anayeimudu vema nafasi hiyo," alisema Eymael.

Aliongeza kiungo huyo anayemhitaji ni atakayekuwa na uwezo wa kuanzisha mashambulizi kuanzia chini kuelekea juu.

"Msingi wa timu siku zote unaanzia chini, ninamaanisha unapokuwa na namba sita makini, atakayetimiza majukumu yake, basi kikosi chake kinakuwa kwenye nafasi nzuri ya kukupa matokeo mazuri," alisema Mbelgiji huyo.

Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela alisema sasa klabu itayafanyia kazi mapendekezo yote yaliyowasilishwa na kocha wao kwa sababu wanahitaji kutimiza malengo ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

"Tulipanga kutoingilia majukumu ya kocha, tumemweleza afanye mazungumzo na mchezaji baada ya makubaliano afikishe mezani taarifa kwa ajili ya kuma mchezaji husika mkataba, kama ilivyokuwa kwa Bernard Morrison alivyotua kwa mara ya kwanza," alisema Mwakalebela.

Licha ya dirisha la usajili kutofunguliwa rasmi hapa nchini, tayari Yanga na timu nyingine zinazoshiriki Ligi Kuu zimeanza kuboresha na kuwapa mikataba nyota waliokwenye mipango yao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >